**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**KWA MWAKA 2022/2023**

**ILIYOWASILISHWA NA**

**MHE. SULEIMAN MASOUD MAKAME (MBM) WAZIRI WA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

**JUNI, 2022**

**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**



**MHE. SULEIMAN MASOUD MAKAME (MBM)**

**WAZIRI, WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ZANZIBAR**

**YALIYOMO**

UTANGULIZI ....................................................................1

UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU KATIKA PATO LA TAIFA ..............................................2

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022 ....................................................4

MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022.......5

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.................................................6

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022............................................................12

PROGRAMU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU...............13

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI..........................18

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI.........................................25

CHANGAMOTO.............................................................30

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023............................................................31

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA..............................32

MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023......................................33

PROGRAMU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU............35

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI..........................38

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YAUCHUMIWABULUUNAUVUVI............................................44

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 .....................47

HITIMISHO ....................................................................47

VIAMBATANISHO ............................................................50

KIAMBATANISHO NAM. 1A ..................................................51

KIAMBATANISHO NAM. 1B ..................................................52

KIAMBATANISHO NAM. 2 ....................................................53

KIAMBATANISHO NAM. 3....................................................54

KIAMBATANISHO NAM.4 ....................................................55

KIAMBATANISHO NAM. 5....................................................56

KIAMBATANISHO NAM. 6 ....................................................57

KIAMBATANISHO NAM. 7....................................................58

KIAMBATANISHO NAM. 8A..................................................59

KIAMBATANISHO NAM. 8B..................................................62

KAMBATANISHO NAM. 8C ..................................................64

KIAMBATANISHO NAM. 8D ..................................................65

KIAMBATANISHO NAM. 8E..................................................66

KIAMBATISHO NAM 8F......................................................67

KIAMBATISHO NAM 8G ......................................................70

KIAMBATISHO NAM 8H ......................................................71

KIAMBATISHO NAM 8I ......................................................72

KIAMBATISHO NAM 8J......................................................73

KIAMBATISHO NAM 8K ........................................ ...................74

KIAMBATISHO NAM 8L: ..........................................................75

KIAMBATISHO NAM 8M ..........................................................76

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu lipokee, lijadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambayo yanawasilishwa katika Mfumo wa Programu (PBB).

2. **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki kinachojadili Bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa anaoutoa kwenye maendeleo ya nchi yetu. Shukurani za pekee zimuendee Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuiongoza Zanzibar katika misingi ya umoja, mashirikiano, usalama, amani na utulivu. Hatua hiyo imepelekea utekelezaji mzuri wa malengo ya serikali na maelekezo yake anayoyatoa mara kwa mara katika kuleta maendeleo ya Sekta za Uchumi wa Buluu na Uvuvi na hatimae kukuza Uchumi wa Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kumshauri vizuri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kufikia azma yake ya kuboresha uchumi na maisha ya Wazanzibari. Vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwashauri vyema viongozi wetu na kufanya maamuzi mema yenye hekima na busara katika kuleta maendeleo Zanzibar.

5. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii adhimu kwa dhati kabisa kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid Spika wa Baraza la Wawakilishi, Pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanayoifanya na tunawaombea dua Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

6. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii kwa namna ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, pamoja na Wajumbe wote na Sekretarieti ya Kamati hiyo, kwa miongozo na ushauri waliyotoa kwa Wizara, katika kufanikisha vizuri utekelezaji wa shabaha na malengo ya bajeti ya mwaka 2021/2022, na kuendelea kutusaidia kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023. Napenda kuihakikishia Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo mliyotupatia yamezingatiwa katika ukamilishaji wa bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU KATIKA PATO LA TAIFA**

7. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imetekeleza kwa vitendo miongozo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, ambayo imetoa mwelekeo wa kimkakati wa kuratibu na kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake, kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekamilisha mapitio ya Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2022, pamoja na rasimu ya mpango mkakati wa Uchumi wa Buluu, kwa lengo la kutekeleza malengo ya Dira ya maendeleo ya Zanzibar ya 2050 ili kusimamia ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

8. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uchumi wa Buluu Zanzibar inajumuisha maeneo mengi ya utekelezaji. Hata hivyo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inawajibika moja kwa moja kwenye sekta ya Uvuvi, Ukulima wa Mwani, ufugaji wa Mazao ya Baharini, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuweka miundombinu na teknologia bora katika kuendeleza sekta hizo. Aidha, Wizara ina jukumu la kuratibu

maendeleo ya Uchumi wa Buluu kwenye sekta za Utalii Endelevu; Usafiri wa Baharini, Usafirishaji wa Bidhaa, pamoja na Miundo Mbinu ya Sekta ya Bahari; na Uratibu wa Usimamizi wa Mazingira ya baharini “Maritime Governance”.

9. **Mheshimiwa Spika,** Mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa ni asilimia 5.1 kwa mwaka 2021. Mchango wa Sekta ya Uvuvi kwa thamani ya pato la Taifa umeongezeka kutoka **TZS 206.4** Bilioni kwa mwaka 2020 hadi kufikia **TZS 236.8** Bilioni kwa mwaka 2021. Aidha, uvuvi wa samaki umeongezeka kutoka tani 38,107 mwaka 2020 hadi tani 47,110 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 19.1. Usafirishaji wa mazao ya baharini ikiwemo majongoo bahari, kaa na pweza umeongezeka kutoka tani 12,167 mwaka 2020 hadi tani 19,064 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 36 **(Kiambatanisho Nam. 1A)**. Usafirishaji wa mwani kipekee nje ya nchi umeongezeka kutoka tani 11,383 mwaka 2020 hadi tani 12,124 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 6.1 **(Kiambatanisho Nam. 1B).**

10. **Mheshimiwa Spika,** Ukuaji wa mchango wa sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa unategemewa kuongezeka zaidi kutokana na juhudi kubwa zilizofanyika hivi karibuni ambapo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetoa jumla ya **TZS Bilioni 36.5** kwa kutekeleza programu ya kuleta ahueni ya janga la UVIKO 19. Taratibu za manunuzi ya zana za Uvuvi (Boti, mashine, mitego, mabwawa, tai tai, kamba) zimekamilika na mafunzo kwa wadau wa sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi yanaendelea Unguja na Pemba. Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajia ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni 2022, Wizara inatarajia kufikia hatua kubwa ya upokeaji wa vifaa na kuanza mchakato wa kuvitoa kwa wananchi.

11. **Mheshimiwa Spika,** Kazi ya matayarisho ya Mpango Mahsusi wa Matumizi ya maeneo ya Bahari (Marine Spatial Planning) imeanza katika hatua za awali Kwa utoaji wa mafunzo kwa wadau wakiwemo wajumbe wa Kamati ya Uchumi na Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Mafanikio ya Uchumi wa Buluu yanategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa mpango wa matumizi ya bahari ambapo utekelezaji wake utawezesha kusimamia uhifadhi bora na thabiti wa maeneo ya bahari, kuvutia uwekezaji na kupunguza migogoro. Utekelezaji halisi

wa “Marine Spatial Planning” utatekelezwa kwa awamu na kwa mashirikiano na wadau wa maendeleo kuanzia mashauriano ya wadau, elimu na uelewa, uwezeshaji, utafiti, hadi kufikia ukamilishaji wa ramani nzima ya mpango wa utekelezaji.

12. **Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyofahamu nchi yetu ipo katika hatua za awali za tafiti zitakazotupa taarifa sahihi kuelekea kwenye uchimbaji wa rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia. Hivyo, kuhusu mchango wa sekta ya Mafuta na Gesi Asilia bado tunahitaji kufanya kazi ya ziada kukamilisha tafiti za kupatikana kwa taarifa hizo za Mafuta na Gesi; na kufanya kazi kwa kushirikiana na Makampuni yenye uzoefu wa sekta hiyo duniani. Kwa hivi sasa Wizara kupitia timu ya majadiliano ya Serikali imeendelea na hatua nzuri za majadiliano na kampuni ya Schlumberger ya kutoka Ufaransa kwa ajili ya kuendeleza tafiti za upatikanaji wa taarifa za kina (Multi Client Seismic Survey) pamoja na matumizi ya taarifa zenyewe za kitaalamu.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022**

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya 2050, ILANI ya Uchaguzi ya CCM, Mpango wa Maendeleo Zanzibar (ZADEP), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), pamoja na Sera na Mipango Mikakati ya Kisekta ya Uchumi wa Buluu. Utekelezaji wa Mikakati na Malengo hayo kumepelekea kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wavuvi, wakulima wa mwani, na wafugaji wa mazao ya baharini. Aidha, mikakati hiyo imesaidia kujenga uelewa kwa taasisi za Serikali na sekta binafsi pamoja na wananchi kwa ujumla kuhusu uwekezaji na uwezeshaji katika sekta ya Uvuvi, Mwani, Mazao ya Baharini, Utafiti, uhifadhi wa maeneo ya bahari, na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imetekeleza malengo yake kupitia Programu Kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;

ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi;
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**15. Mheshimiwa Spika,** Kupitia programu hizo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilipanga kutekeleza jumla ya Miradi saba (7) kama ifuatavyo:

| S/N | JINA LA MRADI | MFADHILI | FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) | BENKI YA DUNIA | 4,606,635,000 |
| 2. | Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP) | IFAD | 10,506,456,000 |
| 3. | Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu Dagaa Kama | SMZ ZAFICO | 4,277,607,000 |
| 4. | Mradi wa ujenzi wa kituo cha kusarifu na uhifadhi wa bidhaa za samaki Malindi | SMZ ZAFICO | 8,292,000,000 |
| 5. | Mradi wa Kuanzisha Uvuvi wa Matenga (Fish Cage Farming) | SMZ ZAFICO | 463,800,000 |
| 6. | Mpango wa IMF wa Ahweni ya UVIKO19 ya uwezeshaji wadau wa sekta ya Uvuvi (Boti, mwani, dagaa, ufugaji wa kaa na majongoo). | SMZ/IMF | 36,500,000,000 |
| 7. | Mradi wa Ujenzi wa Diko na Soko la Malindi. | JICA na SMZ | 24,741,600,000 |

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA2021/2022

**16. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Wizara ilikadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 2,259,412,000** kutoka vianzio vyake 4 vya Unguja na Pemba ikiwa ni pamoja na Ada za uvuvi, Ada ya mazao ya baharini, Mapato ya uvuvi wa Bahari kuu na Ada ya uingiaji wa wageni katika hifadhi za maeneo ya bahari. Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2022, Wizara imekusanya jumla ya **TZS**

**1,233,282,687** sawa na asilimia 54.6 ya makadirio ya miezi tisa. **(Kiambatisho Nam 2).**

17. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliidhinishiwa kutumia **TZS 82,021,831,000** kwa kazi za kawaida na kazi za Maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS 58,542,991,000** kupitia bajeti na **TZS 23,478,840,000** ni uhaulishaji wa nyongeza ya Bajeti kwa kazi za Maendeleo mchango wa SMZ. Hadi kufikia Machi, 2022, fedha zilizoingizwa ni **TZS 38,677,137,805** ambazo ni sawa na asilimia 47.1 (Kiambatisho 3). Kati ya fedha hizo **TZS 3,880,762,168** ni kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo **TZS 1,770,174,010** ni Mishahara, **TZS 1,102,890,428** Matumizi mengineyo na **TZS 1,007,697,730** ni RUZUKU kutoka SMZ. Aidha, fedha za Ruzuku, **TZS 72,544,000** ni kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini; **TZS 789,720,870** ni kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Uchimbaji na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia, na **TZS 145,432,860** kwa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa fedha za Maendeleo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliidhinishiwa **TZS 76,367,131,000.** Hadi kufikia mwezi wa Machi, Wizara imepata **TZS 34,796,375,637** sawa na asilimia 45.6 kwa fedha zilizopangwa miezi tisa. Aidha, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia iliidhinishiwa **TZS 3,000,000,000** na imeingiziwa jumla ya **TZS 380,000,000** ambazo ni Mtaji zikiwa ni asilimia 12.6 ya fedha zilizopangwa kwa kipindi cha miezi tisa.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

19. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2021/2022, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilitekeleza programu zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:

**MAFANIKIO KWA MWAKA 2021/2022**

i. Wizara imesimamia ukusanyaji wa takwimu za uvuvi ambapo kwa kipindi cha Januari hadi Disemba 2021

jumla ya tani za samaki 47,110 zenye thamani ya TZS 236.8 Bilioni zimevuliwa. Kiwango hicho ni ongezeko la wastani wa asilimia 19% ukilinganisha na kiwango cha uvuvi kwa mwaka 2020.

ii. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeipatia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi jumla ya **TZS Bilioni 36.5** kutoka katika mfuko wa Fedha za Ahweni ya UVIKO19 za IMF. Kati ya fedha hizi **TZS Bilioni 2.5** imehamishiwa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa Kiwanda cha mwani Chamanangwe Pemba. Fedha zilizobaki ambazo ni **TZS Bilioni 34** zimekuwa zikitumika na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kuleta Mafanikio yafuatayo:

- Wizara imesaini jumla ya mikataba kumi na mbili (12) kwa ujenzi wa boti 277 za mita 8, boti 300 za mita 7, na boti 500 za mita 5. Vilevile, Mikataba ya ujenzi wa mabwawa 100 ya ufugaji wa majongoo bahari na ujenzi wa vizimba 60 vya ufugaji wa kaa imesainiwa, Matokeo ya utekelezaji wa mikataba hiyo ni:

- Wizara imepokea jumla ya boti 250 za mita 5 kwa ajili ya wakulima wa mwani, na asilimia 20 ya vifaa vya ukulima wa mwani (tai tai, na kamba). Aidha, vifaa vilivyobakia na ambavyo vimeanza kupokelewa ni sehemu ya boti 577 za uvuvi, sehemu ya mabwawa 100 ya ufugaji wa majongoo bahari, sehemu ya mabwawa 60 ya ufugaji wa kaa halikadhalika. harakati za ujenzi wa mabwawa 40 ya ufugaji wa samaki zimeanza.

- Kupitia programu hio, Wizara inaendelea na shabaha ya kuwafikia wananchi 31,770 ambapo ni wadau wa sekta ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini kwa Unguja na Pemba ambao wanatarajiwa kunufaika na mafunzo kuhusu Uchumi wa Buluu, Uekezaji na Shughuli za Uvuvi na Ufugaji wa mazao ya Baharini.

iii. Wizara imeshiriki vikao muhimu vitatu vya “Strategic Dialogue” na Washirika wa Maendeleo, hususan katika

maeneo ya Uchumi wa Buluu, pamoja na wadau wa Umoja wa Ulaya, Mabalozi walio Tanzania, pamoja na Mashirika mengine ya Maendeleo ya Kimataifa. Vikao hivi vilivyofanyika Dar es Salaam chini ya uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano viliisaidia Wizara kuwasilisha mwelekeo wa mashirikiano ya kitaasisi, ubia, mikopo na misaada, katika utekelezaji wa mipango na mikakati yake ya Uchumi wa Buluu kwa ujumla.

iv. Mnamo Disemba mwaka 2021, Wizara iliandaa "Round Table Discussion" Zanzibar na washirika wa maendeleo pamoja na mabalozi wa nje walio Tanzania iliyodhaminiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP); na ahadi mbali mbali zimetolewa za mashirikiano baina ya Wizara na Washirika hao ikiwemo UNDP, UN Women, Norway, Finland, Sweden, Ireland, France, European Union, KOICA, WIOMSA.

v. Wizara imekutana na wawakilishi wa Umoja wa Ulaya walio Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuangalia maeneo ya mashirikiano na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na hasa katika utekelezaji wa mpango wa "EU Green Deal" pamoja na "Team Europe Initiative" na kuisaidia Zanzibar na mpango wake wa Uchumi wa Buluu kupitia programu hizo. Timu ya washauri elekezi wa EU tayari walifika Wizarani katika utekelezaji wa tathmini ya awali "Scoping Study" ya vipaumbele vya mashirikiano baina ya EU na Zanzibar katika Sekta ya Uchumi wa Buluu.

vi. Wizara imeshiriki kwa ukamilifu katika uandaaji wa mradi mpya wa Uchumi wa Buluu kupitia Benki ya Dunia(Tanzania Scaling Up Sustainable Fisheries and Aquaculture Management Project) wenye thamani ya USD Milioni 112 kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kati ya fedha hizo, Zanzibar inatarajia kupata kiasi cha fedha zipatazo USD Milioni 39.

Vilevile, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inaendeleza hatua mbali mbali za matayarisho ya utekelezaji wa miradi

mipya midogo midogo inayochangia katika uwezeshaji na uhifadhi wa mazingira ya bahari kama vile Mradi wa Great Blue Wall Initiative (Tanga Pemba Seascape) unaofadhiliwa na Serikali ya Ireland na unaotekelezwa na Shirika la IUCN. Wizara pia ni mdau wa Mradi wa SAPPHIRE unaofadhiliwa na UNEP Nairobi Convention na FAO-SWIOFC ambao kwa hapa Zanzibar unasimamiwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Halikadhalika, Wizara inashiriki katika Mradi wa World Bank Pro-Blue wa udhibiti wa taka za plastiki baharini (Marine Litter and Microplastics) ambao upo katika ngazi ya tathmini ya awali "scoping study". Na kwa hapa Zanzibar Mradi huo wa Pro-Blue unasimamiwa na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Pia Wizara inashirikiana na WIOMSA katika programu mpya ya masuala ya kupambana na uvuvi haramu (IUU on Small Scale Fisheries) pamoja na mapitio ya usimamizi endelevu wa maliasili za ufukweni na baharini (ICZM Review).

vii. Tarehe 21 Machi 2022, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pamoja zilizindua Mradi wa Meli ya Pacific Star ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania. Mnamo Januari 2022, Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania (DSFA) iliingia makubaliano na Kampuni ya ALBACORA Group ya Uhispania kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu. Pamoja na mambo mengine, ALBACORA Group tayari imesajili kampuni iitwayo PEMBA TUNA LIMITED, na kusajili ZMA meli ya uvuvi, PACIFIC STAR.

viii. Katika Sekta ya Mafuta na Gesi, Wizara inaendelea na ufuatiliaji wa shughuli zinazotekelezwa na mkandarasi ambaye ni RAKGas katika mpango wa ulipaji wa fidia kwa waathirika wa zoezi la Mtetemo, Ukaguzi wa Mkataba (PSA Audit) kwa ajili ya kudhibiti gharama zinazotumiwa na Mkandarasi na kufanya matayarisho ya zoezi la mtetemo wa kina (3D Seismic Survey) kwa ajili ya kutoa mwelekeo wa uchimbaji wa kisima cha utafiti.

ix. Wizara imekamilisha zoezi la Ukaguzi wa Mkataba wa PSA (PSA Audit) kwa Kitalu cha Pemba – Zanzibar na RAKGas na imo katika hatua ya kuandaa ripoti kwa ajili ya kuiwasilisha Serikalini.

x. Wizara imesimamia zoezi la zabuni la kutafuta kampuni itakayofanya utafiti wa pamoja wa Mafuta na Gesi Asilia katika maeneo ya bahari ya mashariki ya Zanzibar ili kuweza kupata taarifa zitakazosaidia katika ugawaji wa vitalu na ufunguaji wa maeneo mapya ya uwekezaji. Aidha, Mamlaka ya ZPRA inaendelea na hatua ya kufanya majadiliano na Kampuni ya Schlumberger kwa ajili ya Uchukuaji wa Taarifa za pamoja kwa njia ya Mtetemo. Aidha, Majadiliano hayo baina ya SMZ na Kampuni ya Schlumberger yanatarajiwa kukamilika karibuni kwa mujibu wa makubaliano yaliyoafikiwa.

xi. Watendaji wa Usimamizi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia wamekuwa wakishiriki Mikutano ya Programu za APDM zinazofadhiliwa na Serikali ya Norway kwa njia ya Mtandao kwa kadri fursa za mafunzo hayo zinavyopatikana.

xii. Kampuni ilifanya vikao vitatu kujadili ulipaji wa fidia kwa waathirika wa zoezi la utafutaji wa awali wa mafuta na gesi asilia kwa njia ya mitetemo (2D) na Mkandarasi RakGas. Aidha Kampuni ilishiriki kikamilifu katika zoezi la uhakiki na ugawaji fomu za malipo ya fidia kwa waathirika wa zoezi la utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa njia ya mitetemo (2D Seismic Survey).

xiii. Kukamilisha ukarabati wa masoko ya samaki ya Tumbe Pemba; na Nungwi Unguja, kupitia mradi wa SWIOFISH

xiv. Kukamilika kwa kazi ya majaribio ya ufungaji wa pweza katika maeneo ya Michamvi/Uroa na Pujini kwa mafanikio.

xv. Kampuni ya ZAFICO kupitia mashirikiano na Benki ya Amana imenunua boti nne (4) za uvuvi na vifaa pamoja na mashine 16 za boti za uvuvi kwa ajili ya mkopo nafuu kwa wananchi wa Shumba Mjini na Kengeja, Pemba. Tarehe 12 Aprili 2022, Boti na vifaa hivyo vilikabidhiwa kwa wanajamii na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt Hussein Ali Mwinyi.

xvi. Kampuni ya ZAFICO imetia saini makubaliano na kampuni ya HAIRU ENGINEERING COMPANY na kuweza kuanzisha miradi ya maendeleo ikiwemo.

- ZAFICO-Hairu Naval Craft Engineering Limited yenye lengo la kujenga kiwanda cha kutengeneza boti pamoja na chelezo katika eneo la Mkokotoni fungurefu Unguja.

- ZAFICO - Hairu Fisheries and Trading Limited, lengo la kampuni hii ni kuendesha shughuli za uvuvi wa bahari kuu, shughuli za uhifadhi wa bidhaa katika vyumba baridi na uzalishaji wa barafu.

- ZAFICO Food Technology Limited: lengo la kampuni hii ni kujenga kiwanda cha kusindika samaki halisi (fresh fish), samaki wa kugandisha kwa barafu, samaki wa kopo, samaki wa kavu, mafuta ya samaki na chakula cha samaki.

xvii. Kampuni ya ZAFICO imenunua mtego mpya, kuufunga na kufanya marekebisho baadhi ya vifaa vya meli na kufanya ukaguzi wa meli ya pili SEHEWA 3 ambapo ujenzi wa meli hiyo umekamilika na meli hio imewasili Zanzibar.

xviii. Wizara kupitia ZAFIRI inatekeleza kipengele cha mradi wa Bluegrasi katika kuwapokea na kuwatunza samaki wazazi aina ya tasi na kolekole kwa lengo la kuzalisha samaki hao. Aidha hadi kufikia mwezi wa Machi kituo kina jumla ya Tasi wazazi 156 na Kolekole wazazi 147.

xix. Kuendelea na kutayarisha Mpango Mkakati wa miaka 5 wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini, pamoja na kuandaa taratibu za hatua za kufanya utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (Standard Operating Procedures)

xx. Kukamilika kwa rasimu ya Sera na Mpango mkakati wa Uchumi wa Buluu, pamoja na Rasimu ya Sera na Sheria ya Uvuvi. Rasimu ya Sera na Sheria ya Uvuvi zimewasilishwa katika Secretarieti ya kamati ya makatibu wakuu kwa kupatiwa maoni.

xxi. Wizara imeandaa andiko la awali "Concept Note" inayohusu kuangalia hali halisi ya kimazingira ya bahari ya eneo la

Mwana wa Mwana ili kulifanya kuwa eneo tengefu (No take zone) litakaloleta tija zaidi na manufaa katika kukuza mapato ya kitalii yanayotokana na hifadhi tengefu za maeneo ya bahari.

xxii. Jumla ya programu 59 kwa taasisi na wananchi kwa jumla zimeendeshwa kwa lengo la kutoa uelewa na fursa zinazopatikana katika Uchumi wa Buluu.

xxiii. Kufanyika vikao vinne vya mashirikiano ya kitaasisi baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya SMT, Wizara ya Nishati ya SMT na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ya SMZ. Kati ya vikao hivyo, vikao viwili ni kati ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Wizara ya Nishati ya SMT na vilizungumzia masuala ya Mafuta na Gesi Asilia; na vikao viwili baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya SMT na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ambavyo vilizungumzia maendeleo ya sekta ya Uvuvi Tanzania.

xxiv. Kukamilika kwa ujenzi wa ofisi (Partition) na uwekaji wa samani za ofisi ya Wizara ndani ya jengo la ZURA, Maisara. Hatua hiyo imewezesha kuweka mazingira bora ya kazi.

xxv. Doria shirikishi 283 zimefanyika katika maeneo ya hifadhi MENAI, MIMCA, CHABAMCA na PECCA kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu (Nyavu za macho madogo, bunduki na madema ya waya) unaopelekea uharibifu wa Mazingira ya Bahari pamoja na kuangalia leseni za vyombo na wavuvi. Aidha, kutokana na doria hizo matokeo 31 (18 Unguja na 13 Pemba) yaliyohusiana na uvuvi haramu yameripotiwa vituo vya polisi na mashauri yao yamehukumiwa nje ya mahakama kwa kutozwa faini ya Jumla ya TZ Milioni 26,700,000. Aidha, wavuvi wote hao walipewa taaluma juu ya utumiaji wa rasilimali za bahari.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**20. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Programu zake kuu tatu (3) na Programu ndogo sita (6) ni kama ifuatavyo:

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

21. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu dhumuni lake kubwa ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Programu hii ina programu ndogo moja nayo ni Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na ina huduma mbili kama ifuatavyo:

i. Uratibu wa Uchumi wa Buluu
ii. Udhibiti wa ufuatiliaji na uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

22. **Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu hii iliombewa **TZS 2,447,800,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **TZS 799,800,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 1,648,000,000** ni Ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2022, Programu imepata jumla ya **TZS 1,023,495,856** sawa na asilimia 42%. Kati ya Fedha hizo, **TZS 233,774,986** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 789,720,870** ni Ruzuku kutoka Serikalini.

**Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu.**

23. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu kupitia huduma ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu inalenga kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2021/2022 kwa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu**

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kukamilisha kuandaa Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2022. Ukusanyaji wa maoni ya wadau umekamilika na Sera imewasilishwa kwenye vikao vya Makatibu Wakuu kwa mujibu wa utaratibu.

ii. Kukamilisha Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu Zanzibar.

iii. Kukamilika kwa mpango wa kuwawezesha wadau wa sekta ya Uvuvi “Blue Economy Intervention Plan”.

iv. Kukamilisha programu 48 kwa taasisi binafsi na Serikali za kujenga uelewa na kuainisha fursa zinazopatikana katika uchumi wa buluu.

v. Wizara imefanikiwa kuratibu na kuhudhuria jumla ya mikutano kumi na saba (17) yenye lengo la kukuza Sekta ya Uchumi wa Buluu ndani na nje ya Zanzibar.

vi. Watendaji wamepata fursa za kujenga uelewa na mashirikiano na taasisi za nje ya Zanzibar ikiwemo Namibia, Uingereza, Ufaransa, Ubelgiji, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ghana, Kenya, Korea ya Kusini, Reunion, na Afrika ya Kusini.

vii. Kupitia Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Wizara imeshirikishwa katika michakato ya usimamizi wa madini ya ardhi ya baharini (Seabed) huko Jamaica; na katika vikao vya uandaaji wa mkataba mpya wa usimamizi wa bioanuwai katika bahari kuu iliyo nje ya mipaka ya kimataifa (ABNJ).

viii. Wizara imeshiriki katika Kongamano la biashara kati ya Tanzania na Uingereza; makongamano ya Uchumi wa Buluu pamoja na UNDP, UN Women, Ufaransa na Uongozi Institute; Mashirikiano na Taasisi ya AU-NEPAD kuhusiana na uvuvi na kilimo cha mwani; Kupitia mapendekezo ya Mkataba wa Utatu wa Biashara kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, COMESA na SADC; Mikutano na Warsha za mitandao kupitia IOTC, IORA, Jamhuri ya Watu wa China, n.k. Wizara imeshirikiana na Taasisi ya Tony Blair Institute katika kujenga uwezo wa kuwa na vipaumbele vya utekelezaji wa Uchumi wa Buluu; Kuandaa utaratibu wa kuanzisha Mpango maalum wa matumizi ya maeneo ya Bahari kwa mashirikiano na UNDP, Norway, UN Women, na TNC.

**25. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu iliombewa

**TZS 799,800,000** kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2022, Programu ndogo hii imepata jumla ya **TZS 233,774,986** kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatisho 3)** ambayo ni sawa na asilimia 29.2 kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA)**

26. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ni taasisi yenye jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

27. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu hii ilitekeleza na kufanikisha shabaha zifuatazo:

i. Kuandaa Kanuni nne (4) kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za Mafuta na Gesi Asilia. Kanuni hizo ni "Petroleum General Regulations", Kanuni ya Thamani ya Wadau (Local Content Regulations), Kanuni ya Afya, Usalama na Mazingira (Health Safety and Environment Regulations) na Kanuni ya Fedha (Financial Regulations).

ii. Kuendesha programu 31 kwa ajili ya kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu masuala ya Mafuta na Gesi. Kati ya programu hizo, Programu moja (1) ilifanyika kwa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi. Programu kumi na sita (16) zilifanywa katika Taasisi za Serikali Unguja (7) na Pemba (9). Programu nane (8) zimefanywa katika vyombo vya Habari (ZBC TV, ZBC Radio, Magazeti na Bahari FM na ZCTV). Programu mbili (2) zimefanyika kwa Mabaraza ya Vijana Mikoa ya Kusini (1) na Kaskazini (1), programu mbili (2) zimefanyika kupitia mikutano ya wanashehia wa Kama na Kidimni kuhusiana na suala la fidia; Programu moja (1) ilifanyika kwa ajili ya maonesho ya Biashara katika wiki ya Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar; na progamu moja (1) ilifanyika kwa ajili ya sherehe za utiaji saini MoU baina ya ZPRA na PURA.

iii. Kuendelea kusimamia zoezi la utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa kitalu cha Pemba - Zanzibar.

iv. Mamlaka imefanikiwa kuendesha shughuli 36 za ufuatiliaji ikiwemo ziara kumi na nne (14) na mikutano/ vikao ishirini na mbili (22).

v. Ziara kumi (10) zilifanywa kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala ya ulipaji fidia kwa waathirika wa mazao na nyumba wakati wa zoezi la Mtetemo kwa Unguja na Pemba kwa ajili ya kuhakiki malipo ya ulipaji wa fidia kwa wahusika.

vi. Kamati ya Uchumi ya BLW imetembelea TPDC - Dar es Salaam na Kisima cha Pemba – 5 kilichopo Tundaua Pemba.

vii. Kufanyika kwa jumla ya vikao 19 baina ya ZPRA, Kampuni ya ZPDC na RAKGas kuhusu masuala ya ulipaji fidia kwa waathirika wa mazao na nyumba wakati wa zoezi la Mtetemo kwa Kitalu cha Pemba – Zanzibar.

viii. Wizara imekamilisha zoezi la Ukaguzi wa Mkataba wa PSA (PSA Audit) kwa Kitalu cha Pemba – Zanzibar na imo katika hatua ya kuandaa ripoti kwa ajili ya kuiwasilisha Serikalini.

ix. Kusimamia zoezi la utafiti wa pamoja (Multi client) wa Mafuta na Gesi Asilia katika maeneo ya bahari ya mashariki ya Zanzibar ili kuweza kupata taarifa zitakazosaidia katika ugawaji wa vitalu na ufunguaji wa maeneo mapya ya uwekezaji.

**28.** **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imetekeleza mambo matano (5) ambayo ni kukamilisha uandaaji wa nyaraka tatu (3) muhimu zilizotumika kwa ajili ya utoaji wa Zabuni, kutangaza Zabuni ya Uchukuaji wa Taarifa za Pamoja kwa njia ya Mtetemo (Multi- client Seismic Survey), kukamilisha kazi ya kufanya Tathmini ya zabuni ya multi-client kwa maeneo yote mawili ya maombi ya kitaalamu na kifedha (Technical & Financial proposal), kuwasilisha Serikalini Ripoti ya kazi ya kufanya Tathmini maombi ya zabuni ya Multi –client kwa ajili ya

mazingatio pamoja na kukamilisha majadiliano na Kampuni ya Schlumberger iliyoshinda Zabuni hiyo.

x. Kuendelea kuimarisha na kusimamia Mfumo wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia, Wadau wa Sekta pamoja na kutoa taarifa na machapisho zinazohusiana na shughuli za Mafuta na Gesi Asilia.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza lengo hili, Mamlaka imefanikiwa kuwapatia mafunzo manne (4) ya muda mfupi na mafunzo mawili (2) ya muda mrefu yaliyopangwa kwa wafanyakazi wa Mamlaka. Vile vile Mamlaka imeweza kukamilisha mapendekezo ya kujaza nafasi katika Muundo wa Mamlaka (Organization Structure) baada ya kuridhiwa na Serikali, kukamilisha Rasimu ya Muundo wa Utumishi wa Mamlaka (Scheme of Service) na kuingia Hati ya Makubaliano baina ya ZPRA na PURA.

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia iliombewa **TZS 1,648,000,000** kwa kazi za kawaida. kati ya hizo **TZS 1,096,300,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **TZS 551,700,000** ni Mishahara ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini . Hadi Machi 2022, Mamlaka imepatiwa jumla ya **TZS 789,720,870** ambapo **TZS 340,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na **TZS 449,720,870** ni Mishahara sawa na asilimia 47.9% ya fedha zilizoombwa.

**Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (ZPDC)**

31. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia ina jukumu kubwa la kushiriki katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kufanya biashara katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa niaba ya Serikali na kulinda maslahi ya Taifa katika biashara ya Mafuta na Gesi Asilia.

**Utekelezaji wa Shabaha za Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Mwaka 2021/2022**

Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia imeweza kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kujenga uwezo kwa Watendaji wa Kampuni katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia;

ii. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa watendaji wa Kampuni ya ZPDC kwa kuwapatia watendaji wa Kampuni vifaa vya kufanyia kazi, vifaa vyenyewe ni Laptop nne (4), Desktop nne (4), Kamera mmoja (1) na Vifaa vyenginevyo (Accessories).

iii. Kuongeza Wafanyakazi 3 katika fani ya Uhandisi wa Mafuta na Gesi (Petroleum Engineer), Utaalamu wa miamba (Geologist) na Utaalamu wa Usalama, Afya na Mazingira katika shughuli za mafuta na gesi asilia.

iv. Uendeshaji wa shughuli za Mkataba wa mgawanyo wa Mafuta na Gesi Asilia (PSA);

v. Kutoa uelewa wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi za Serikali na wananchi.

vi. Kukamilika na kusainiwa kwa Makubaliano ya Ushirikiano (MOU) kati ya Kampuni ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

vii. Kukamilika kwa Mpango Kazi wa biashara ya Ununuzi wa Nishati ya Mafuta kwa Pamoja kwa visiwa vya Unguja na Pemba (Petroleum Bulk Procurement Business case in Zanzibar).

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia ilitenga **TZS 3,000,000,000** kwa kazi za kawaida. Hadi Machi 2022, Kampuni imetumia jumla ya **TZS 773,400,784.** Kati ya fedha hizo **TZS 441,628,657** ni Mishahara na **TZS 331,772,127** zilitumika kwa Kazi za Uendeshaji sawa na asilimia 25.7% kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI**

33. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini inalenga kuendeleza uvuvi wa

kienyeji na kusimamia shughuli zote za ufugaji wa samaki na ukulima wa mazao mengine ya baharini pamoja na kuimarisha ubora na thamani ya mazao ya baharini. Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari;

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu hii iliombewa **TZS 77,800,746,000** ambapo **TZS 538.19** millioni ni mishahara, **TZS 596.32** millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 299.1** millioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti. Vilevile, **TZS 76,367,131,000** ni kwa ajili ya fedha za Maendeleo ambapo **TZS 40,112,440,000** ni kutoka SMZ, na **TZS 36,254,691,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2022, Programu hii imepata jumla ya **TZS 36,368,973,233** sawa na asilimia 47% Kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS 842,387,115** ni mishahara, **TZS 512,233,621** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 217,976,860** ni Ruzuku kutoka Serikalini. Aidha **TZS 34,796,375,637** ni kwa ajili ya fedha za Maendeleo, ambapo **TZS 32,360,949,614** mchango wa SMZ na **TZS 2,435,426,023** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. **(Kiambatisho 4.)**

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Mazao ya Baharini**

35. **Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi ina lengo la kusimamia na kuendeleza uvuvi pamoja na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2021/2022 kwa Programu ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa mazao ya Bahari:**

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendeleza kilimo cha mwani na kuongeza uzalishaji kutoka tani 9,000 hadi zaidi ya 12,000 kwa kuwapatia wakulima mafunzo bora ya uzalishaji wa mwani na

kuwapa nyenzo zitakazosaidia kufanya usarifu wa mwani.

ii. Jumla ya vikundi 150 vya wakulima wa mwani vimepatiwa mafunzo (Unguja 90 na Pemba 60) kuhusu njia bora za kisasa za upandaji mwani yenye uwezo wa kuongeza uzalishaji wa mwani mara tatu hadi nne.

iii. Jumla ya mashamba darasa ya mfano 10 ya mwani yameanzishwa katika vijiji 10 vya Unguja (Matemwe, Mwambale, Muyuni A, Kizimkazi, Ukongoroni, Kisakasaka, Bweleo, Fujoni, Kiongwe na Pongwe.) ili kuweza kuwapa fursa ya kujifunza wakulima wa mwani.

iv. Majaribio ya kuzalisha mwani wa aina ya cottonii kijiji cha Mwambale yanaendelea vizuri, mwani unaozalishwa unasambazwa kama mbegu hapo kijijini na baadae kusambazwa kwenda vijiji vyengine ili kuongeza uzalishaji wa mwani wa jamii ya cotonii.

v. Jumla ya vikundi 131 (Unguja 73 na Pemba 58), vimepatiwa mafunzo ya ufugaji wa mazao ya baharini.

vi. Wafugaji 180 wakiwemo 50 kutoka Pemba na 130 kutoka Unguja wamepatiwa mafunzo ya ufugaji wa majongoo bahari.

vii. Jumla ya samaki aina ya Tasi wazazi 152, Kolekole wazazi 147 wanaendelea kutunzwa kituoni kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Kituo cha kutotolesha vifaranga vya Samaki kimefanikiwa kuzalisha vifaranga vya Samaki 19,473 vya sato na kambare 39,394 na kuvisambaza kwa wanajamii.

viii. Kuwawazesha wavuvi wadogo wadogo 150 (Unguja 75 Pemba 75) kuweza kuvua kwenye maji ya kina kirefu kwa kuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na taasisi za mikopo kuweza kupatiwa mikopo. Jumla ya wavuvi 5770 wameanza kuunganishwa na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupatiwa boti 577 kupitia programu ya ahueni ya UVIKO 19.

ix. Ujenzi wa diko na soko la kisasa la samaki la Malindi umefikia asilimia sabini na tatu (73%). Soko hilo litaweza kuhudumia jumla ya wafanya biashara 6500 na litakuwa na vyumba vya baridi vyenye uwezo wa wastani wa tani 200.

**37. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu ndogo hii iliombewa **TZS 77,500,746,000.** Kati ya hizo, **TZS 538.19** millioni ni kwa ajili ya mishahara, **TZS 296.32** millioni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 299.1 millioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti. Aidha **TZS 76,367,131,000** zilikuwa ni kwa ajili ya fedha za Maendeleo ambapo **TZS 40,112,440,000** zilikuwa kutoka SMZ, na **TZS 36,254,691,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2022, Programu ndogo hii imepata jumla ya **TZS 36,288,545,691** Kwa kazi za kawaida ambapo mishahara ni **TZS 842,387,115**, matumizi mengineyo **TZS 512,233,621** na **TZS 217,976,860** ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti na Kampuni ya Uvuvi ZAFICO. Aidha **TZS 34,796,375,637** ni kwa ajili ya fedha za Maendeleo (ikiwa **TZS 2,435,426,023** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **TZS 32,360,949,614** mchango wa SMZ ikiwemo **TZS 30,027,340,000** za utekelezaji wa Programu ya UVIKO 19 **(Kiambatisho 4).**

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini**

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kukamilika kwa Rasimu ya Sheria ya Taasisi;

ii. Kukamilika kwa Rasimu ya Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa Taasisi wa Miaka mitano;

iii. Kukamilika kwa Rasimu ya Muundo wa Taasisi;

iv. Kitabu chenye taarifa za muhtasari za tafiti 1,016 za Uvuvi na Mazao ya Baharini zilizofanyika Zanzibar kuanzia mwaka 1999-2020 kimekamilika;

v. Kitabu cha Muongozo wa Kitaalamu wa Ufugaji wa Majongoo Bahari Weupe kimekamilika;

vi. Utafiti wa kutambua kipato na matumizi ya Wavuvi na Wachuuzi kwa lengo la kuwa na taarifa za awali (baseline information) umefanyika;

vii. Samaki wazazi aina ya Tasi (156) na Kolekole Sio (100) wamekusanywa kwa ajili ya Utafiti wa uzalishaji wa vifaranga;

viii. Taasisi imefanikisha kuhamia katika Jengo jipya la kisasa lililofadhiliwa na Mradi wa SWIOFish;

ix. Watafiti wamepatiwa mafunzo ya kitaalamu ya kufanya tafiti za Maliasili za baharini na jinsi ya kuandaa maandiko na machapisho ya tafiti;

x. Kukamilisha Rasimu za Kanuni za Matumizi ya Maabara;

xi. Kukamilika kwa Rasimu ya Taratibu za ufanyaji wa Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini (Standard Operating Procedures) kwa Taasisi ya ZAFIRI kwa kushirikiana na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania (COSTECH)

xii. Kushiriki katika majadiliano ya pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ya Tanzania (TAFIRI) juu ya Uvuvi wa Ringnet kwa lengo la kutoa mapendekezo ya kitaalamu juu ya usimamizi wa Uvuvi wa aina hii.

**39. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini iliombewa jumla ya **TZS 299,100,000** milioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2022 Taasisi imepata **TZS 72,544,000** kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 24.2 ya fedha zilizoombwa.

**Kampuni ya Uvuvi Zanzibar – ZAFICO**

**40. Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Kampuni ya Uvuvi ya ZAFICO ni kuanzisha Uvuvi wa kibiashara kwa kuimarisha ujenzi wa Miundombinu ya Uvuvi na kuelekeza nchi katika uchumi wa Buluu.

**Utekelezaji wa Shabaha za Kampuni ya ZAFICO 2021/2022**

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Ununuzi wa meli ya pili ya uvuvi umefanyika na umefikia asilimia 100 ya uundaji na malipo na meli hiyo tayari imeshawasili Zanzibar.

ii. Jumla ya Kilo 578 za samaki aina ya Jodari, Sehewa, Mbasi na Sansuri wamevuliwa na kuingizwa katika soko la Zanzibar.

iii. Kuendeleza utekelezaji wa Miradi wa uanzishwaji wa Kampuni ya Zanzibar Aquaculture Harvest Company (ZAHC) ambapo ukamilishaji wa Hatimiliki (DP2039/2022) ya eneo (Ukubwa wa 2.99ha) la mradi wa uvuvi wa matenga kwa Kampuni ya Zanzibar Aquaculture Harvest Company (ZAHC) umeshafanyika.

iv. Hatimiliki ya eneo la mradi (title deed) imeshakabidhiwa ZAFICO kwa niaba ya Kampuni ya ZAHC. Hatua nyengine za utekelezaji zinazoendelea ni ukamilishaji wa upembuzi wa kimazingira na tathmini ya vipando vya wananchi watakaoathirika na mradi.

42. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) ilitarajia kupata jumla ya **TZS 43.11** bilioni kutoka vyanzo mbali mbali ambapo **TZS 1.29** bilioni kutoka mashirika yenye hisa (ZSSF, ZSTC, ZIC na ZPC) na TZS 785.36 milioni ikiwa ni pato linalotokana na uzalishaji wake. Aidha pamoja na uwekezaji wa jumla ya TZS 13.033 bilioni kutoka SMZ na **TZS 11.327** bilioni kwa washirika wa maendeleo **(TZS 3.15** bilioni IFAD na **TZS 8.18** bilioni kutoka kwa wadau wanaounda kampuni ya ZAHC) . Hadi kufikia Machi, 2022 Kampuni imetumia **TZS 726,444,478** kati ya **TZS 2,046,591,584** zilizopangwa kwa kazi za kawaida na mishahara sawa na asilimia 35.5%. Kwa upande wa miradi ya Maendeleo Jumla ya **TZS 486** Milioni zimeingizwa katika utengenezaji wa chanja za kuanikia dagaa KAMA.

### Programu ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari

43. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uhifadhi wa maeneo ya bahari ina jukumu la kuendelea kuyatunza mazingira ya bahari pamoja na rasilimali zake hususan maeneo ya hifadhi kupitia utoaji wa taaluma, mbinu bora za uhifadhi na doria shirikishi.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2021/2022 kwa Uhifadhi wa Rasilimali za bahari**

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kamati za uvuvi 100 (Unguja 70 na Pemba 30) zilijengewa uwezo ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi ikiwa ni pamoja na kusimamia rasilimali za bahari kwa kuanzisha maeneo ya ufungaji wa pweza na samaki wa miambani.

ii. Kamati 48 zilipata mafunzo ya kufanya uchaguzi wa kamati za uvuvi ili kuweza kupata kamati madhubuti ambazo zitafanya kazi ya usimamizi shirikishi wa maeneo ya baharí na kusababisha kuongeza mazalia ya samaki.

iii. Jumla ya wavuvi 120 kutoka katika hifadhi za MENAI na MIMCA walishiriki Mafunzo juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ya bahari na athari za uvuvi haramu.

iv. Utekelezaji wa zoezi la ufungaji wa maeneo tengefu yalioko katika hifadhi ya TUMCA (mwana wa mwana), MIMCA (Michamvi), na CHABAMCA (kisiwa cha makobe na funguni) pamoja na kukusanya ada ya tozo za makusanyo (dola 3) kwa wageni baada ya kujadiliana na wadau wa utalii na jamii husika.

v. Mafunzo ya uongozi shirikishi (Co-Management) yalitolewa na mshauri elekezi kwa wafanyakazi 30 (15 Unguja na 15 Pemba) kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuandaa mipango ya usimamizi ya uvuvi (Local Management Plan) katika maeneo ya hifadhi za baharí.

vi. Zoezi la kufanya usafi wa fukwe na mafungu lilifanyika katika hifadhi ya CHABAMCA (fungu la "nakupenda" na fungu nyange) na TUMCA katika maeneo ya fukwe, washiriki katika zoezi hili ni wafanyakazi kutoka Idara ya Hifadhi ya Maeneo ya Bahari, wavuvi pamoja na askari jamii.

vii. Doria shirikishi 283 zilifanyika katika maeneo ya hifadhi za MENAI, MIMCA, CHABAMCA na PECCA kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu (Nyavu za macho madogo, bunduki na madema ya waya) unaopelekea uharibifu wa mazingira ya bahari pamoja na kuangalia leseni za vyombo na wavuvi. Aidha kutokana na doria hizo, matokeo 31 (18 Unguja na 13 Pemba) yaliyohusiana na uvuvi haramu yameripotiwa vituo vya polisi na mashauri yao yamehukumiwa nje ya mahakama kwa kutozwa faini ya jumla ya **Tsh 26,700,000/=**. Aidha wavuvi wote hao walipewa taaluma juu ya utumiaji endelevu wa rasilimali za Baharini.

**45. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 programu ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari imeombewa jumla ya **TZS 300,000,000** kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2022 programu ndogo hii imetumia jumla ya **TZS 80,427,542** sawa na asilimia 26.8% ya fedha zilizopangwa.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI.**

**46.Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara, Programu ndogo ya Uendeshaji na Utawala na Programu Ndogo ya Utawala na Ofisi Kuu Pemba.

**47. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022, Programu hii iliombewa jumla ya **TZS 1,773,085,622** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **TZS 1,142,905,622** ni mishahara, **TZS 630,180,000** matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2022 Programu hii imepata jumla ya **TZS 1,284,668,716** kati ya fedha hizo **TZS 927,786,895** mishahara, TZS 356,881,821 kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 72.4% kwa fedha zilizopangwa miezi tisa.

**Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti.**

48. **Mheshimiwa Spika,** Dhumuni la programu hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati na Mipango ya maendeleo na Utafiti, pamoja na kuratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi zikiwemo washirika wa maendeleo na sekta binafsi. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti.

**Utekelezaji wa programu ndogo ya Mipango kwa mwaka 2021/2022 ni kama ifuatavyo:**

i. Marekebisho ya Sera na Sheria ya Uvuvi Nam 7 ya mwaka 2010 yamekamilika na kuwasilishwa kwenye vikao vya makatibu Wakuu. Sheria hiyo imegawika kwenye maeneo matatu yakiwemo Uvuvi; Uhifadhi wa Bahari na Utafiti katika sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

ii. Rasimu ya Sheria ya Mafuta na Gesi imekamilika na kupatiwa maoni ya wadau wa sekta ya Uchumi wa Buluu (Unguja na Pemba). Kwa hivi sasa inafanyiwa utafiti na Tume ya Marekebisho ya Sheria.

iii. Kufanyika vikao vinne vya mashirikiano baina ya Wizara za SMT na SMZ. Kati ya vikao hivyo, vikao viwili (2) ni kati ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Wizara ya Nishati ya SMT na vilizungumzia masuala ya Mafuta na Gesi Asilia.; na vikao viwili (2) baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya SMT na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ambavyo vilizunguzia maendeleo ya sekta ya Uvuvi Tanzania.

iv. Kukamilika kwa tafiti mbili ikiwemo utafiti wa hali ya ukusanyaji wa mapato katika hifadhi ya PECCA, MIMCA, na MENAI na utafiti wa pili ni kuhusu hali ya ukusanyaji wa takwimu za sekta ya Uvuvi.

v. Matayarisho ya miradi mitatu mipya kwa fedha za washirika wa maendeleo zenye thamani ya **TZS 29,555,000,000.** Vilevile, Idara imetayarisha miradi mitano mipya yenye thamani ya **TZS 52,000,000,000** kwa fedha za Serikali ya mapinduzi Zanzibar.

vi. Ufuatiliaji na tathmini wa kazi za Wizara pamoja na Programu na miradi zimefanyika.

vii. Kuratibu ziara na vikao vinne (4) vya kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na kuwasilisha ripoti ya kamati ya Bajeti.

viii. Kukamilisha mafunzo juu ya masuala ya utayarishaji wa Bajeti (MTEF, PBB) kwa maafisa Bajeti/Mipango wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

49. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 programu ndogo ya Mipango na Usimamizi wa kazi za Wizara iliombewa jumla ya ***TZS 250,232,934.*** Kati ya fedha hizo, **TZS 83,932,934** ni mishahara na **TZS 166,300,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2022, programu ndogo hii imepata jumla ya **TZS 177,408,687**. Kati ya fedha hizo, **TZS 84,542,125** ni mishahara na **TZS 92,866,562** ni kwa matumizi mengineyo, ambayo ni sawa na asilimia 70.8% ya fedha zilizopangwa.

**Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji**

50. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Madhumuni ya programu hii ni kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Aidha, programu inaratibu masuala ya haki na wajibu wa wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria na kanuni za utumishi Serikalini pamoja na kuratibu masuala mtambuka ikiwemo Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2021/2022**

51. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji kwa mwaka 2021/2022 ni kama ifuatavyo:

i. Kukamilisha Ukaguzi wa ndani wa mahesabu ya miradi 2 (SWIOfish na Soko na Diko la Malindi) pamoja na Kampuni ya Mendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

ii. Kuandaa jumla ya vipindi 11 vya televisheni ambavyo vipindi nane (8) vilirushwa ZBC, viwili (2) TBC na kimoja Zanzibar Cable TV.

iii. Kufanya manunuzi ya vitendea kazi na samani za Wizara.

iv. Jumla ya wafanyakazi 55 wamepatiwa stahiki zao. Kati ya hao, wafanyakazi 6 fedha za ubani kwa wafiwa, wafanyakazi 27 malipo ya muda wa ziada (overtime) na wafanyakazi 22 fedha za Likizo.

v. Jumla ya wafanyakazi 50 wamepatiwa mafunzo ya awali chuo cha Utawala wa Umma IPA.

vi. Jumla ya watendaji 4 wamekwenda mafunzo ngazi ya Diploma.

**52.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, iliombewa jumla ya **TZS 825,318,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TZS 601,434,000** ni mishahara na **TZS 233,880,000** ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2022, Programu imepatiwa **TZS 662,314,774** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **TZS 423,986,255** ni mishahara na TZS 238,328,519 ni kwa matumizi mengineyo ambayo ni sawa na asilimia 80.2% ya fedha zilizopangwa.

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Uchumi wa Buluu Pemba**

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2021/2022**

**54.** **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa programuu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba kwa mwaka 2021/2022 ni kama ifuatavyo:

i. Kuratibu na kufanikisha ziara tatu (3) na vikao vya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;

ii. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini na vituoni;

iii. Vikao 6 vya uendeshaji na usimamizi wa ofisi kuu Pemba vimefanyika kwa kushirikiana na Idara na taasisi mbali mbali mtambuka za sekta ya Uchumi wa Buluu na uvuvi - Pemba;

iv. Kukamilisha uratibu wa ziara 8 za viongozi wa Wizara na ziara 4 za viongozi wa Kitaifa.

v. Kufanikisha upatikanaji wa mkopo wa mashine 32 za wavuvi kutoka Benki ya CRDB.

vi. Kuratibu kikao cha semina elekezi kwa wavuvi waliopata changamoto mbali mbali nchi jirani.

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 iliombewa **TZS 697,534,688** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TZS 457,534,688** ni mishahara na **TZS 240,000,000** ni matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2022 programu hii imepata **TZS 444,945,255** kwa kazi za kawaida Kati ya fedah hizo, **TZS 419,258,515** ni mishahara na **TZS 25,686,740** ni matumizi mengineyo ambayo ni sawa na asilimia 63.7% ya fedha zilizopangwa.

## CHANGAMOTO

56. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada za Wizara na Serikali kwa ujumla, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza malengo yaliyowekwa ni pamoja na:

| NAM | CHANGAMOTO | HATUA YA KUTATUA CHANGAMOTO |
|---|---|---|
| 1. | Ukosefu wa miundo mbinu ya bandari jumuishi za uvuvi pamoja na viwanda vya kuchakata minofu ya samaki | Wizara imeendelea na jitihada zake za kuandika miradi mbali mbali kupitia washirika wa maendeleo na sekta binafsi pamoja na kutafuta njia za mikopo ya mabenki. |
| 2. | Ukosefu wa miundo mbinu ya kukaushia dagaa, kusarifu mwani na mazao ya baharini. | Wizara inatekeleza programu ya fedha za ahweni ya UVIKO19 za IMF katika kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya kukaushia dagaa na kusarifu mwani pamoja na uimarishaji wa mashamba ya mazao ya baharini kama vile majongoo bahari, kaa na samaki. |
| 3. | Ukosefu wa taasisi ya vipimo na viwango vya mazao ya baharini (Competent Authority) | Wizara imekuwa katika awamu za awali za mipango ya mashirikiano na washirika wa maendeleo kama vile Ufaransa na EU kusaidia kupatikana kwa taasisi hii ya viwango na leseni za mazao ya baharini na utambuzi wake. |
| 4. | Kuendelea kujitokeza kwa Uvuvi haramu na baadhi ya wavuvi kukaidi sheria na kanuni za uvuvi endelevu na hifadhi ya bahari. | Wizara inaendelea kutoa elimu na kutekeleza sheria kwa wavuvi na kuandaa Sera na Sheria mpya za Uvuvi ambazo ni shirikishi na endelevu. |
| 5. | Uwekezaji katika ukanda wa uchumi wa Bahari (EEZ) bado ni finyu | Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania imefanya mazungumzo na washirika wa maendeleo kama EU ili kushajiisha nchi hizo kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu. Pia Mamlaka imeendelea kushirikiana na sekta binafsi kutoka ndani na nje nchi mbali mbali duniani kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu pamoja na miundo mbinu ya mazao ya bahari kuu. |
| 6. | Wawekezaji wengi wanakuja kwa majadiliano na kutofikia hatua ya kuekeza. | Kuendelea kushirikiana na Taasisi za Kitaifa zinazohusiana na uratibu wa uwekezaji, Balozi za Tanzania Nje ya Nchi, pamoja washirika wa maendeleo katika kuvutia uwekezaji zaidi katika Sekta ya Uchumi wa Buluu Zanzibar. |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | COVID 19 imeathiri mnyororo wa thamani wa Sekta ya Uvuvi | Fedha za ahueni ya UVIKO 19 ambazo ni **TZS 36.5 Bilioni** zimeanza kuleta faraja kwa wadau. |
| 8. | Mabadiliko ya tabia nchi yanayopelekea athari za kimazingira. | Elimu inaendelea kutolewa na mazingira na matumizi ya teknolojia sahihi za usimamizi wa bahari. |

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### MAKADIRIO YA MAPATO 2022/2023

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 2,259,412,000** kutoka vianzio vyake 4 vya Unguja na Pemba **(Kiambatanisho Nam. 5).**

### MAKADIRIO YA MATUMIZI 2022/2023

58. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 Wizara inaombewa kutumia jumla ya **TZS 89,662,400,000,** kati ya fedha hizo **TZS 8,107,400,000** ni kwa kazi za kawaida na **TZS 81,555,000,000** kwa kazi za maendeleo. **(Kiambatanisho Nam. 6).**

59. **Mheshimiwa Spika,** Mgawanyiko wa makadirio ya Matumizi ni **TZS 8,107,400,000** za kazi za kawaida. Kati ya hizo **TZS 2,429,800,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **TZS 3,269,800,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 2,407,800,000** ni RUZUKU kutoka SMZ. Kwa fedha za Ruzuku. Kiasi cha **TZS 320,000,000** ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao Baharini, **TZS 1,775, 300,000** ni kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, na **TZS 312,500,000** ni kwa ajili ya Kampuni ya ZAFICO. (**Kiambatanisho Nam. 6).**

60. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, Wizara inaombewa jumla ya **TZS 81,555,000,000.** Kati ya fedha hizo, **TZS 52,000,000,000** kutoka SMZ na **TZS 29,555,000,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

**(Kiambatanisho Nam. 7).** Aidha, Jumla ya **TZS 4.4 bilioni** zimetengwa kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia.

**UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA**

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 itatekeleza malengo yake kupitia Programu zake kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;
ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi;
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

62. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itatekeleza jumla ya miradi nane (8) ya Maendeleo kama ifuatavyo:

i. Mradi wa Ujenzi wa bandari ya Uvuvi, Diko na huduma za masoko Malindi kupitia ufadhili wa Serikali ya Japan

ii. Mradi wa maendeleo ya Uchumi wa Buluu wa Benki ya Dunia kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Tanzania Scaling Up Sustainable Fisheries and Aquaculture Management Project).

iii. Mradi jumuishi wa uwezeshaji wa wanawake katika ukulima wa mwani na ufugaji wa mazao ya baharini kutoka KOICA

iv. Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi kupitia Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD)

v. Mradi wa Ujenzi wa viwanda vya maboti na kusarifu samaki na dagaa wa ZAFICO na Kampuni ya Hairu Naval Craft Engineering Ltd, pamoja na uvuvi wa bahari kuu

vi. Ujenzi wa Bohari ya Gesi (Natural Gas/LPG Storage Facility) pamoja na miundombinu ya usambazaji wa Gesi,

vii. Ujenzi wa Bohari ya Mafuta (Bulk Storage facilities) pamoja na miundombinu ya usambazaji wa mafuta,

viii. Mradi wa Kuanzisha kituo cha kuhifadhi taarifa za mafuta na Gesi Asilia (National Data Repository au NDR)

ix. Programu ya kuleta ahueni ya UVIKO 19

63. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi itaendelea na uwezeshaji wa jamii kwenye miradi ya kuleta ahueni ya UVIKO 19. Aidha pamoja na miradi hio Wizara itashajihisha jamii kupitia Programu ya uwezeshaji ya wadau wa sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi “Blue Economy Intervention Plan”

**MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NAUVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

64. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni Kukuza Uchumi wa Zanzibar kwa kuimarisha matumizi endelevu ya bahari pamoja na kuwawezesha Wajasiriamali ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana, mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya Biashara na Viwanda ambayo itasaidia upatikanaji wa ajira na masoko kwa vijana kupitia Uchumi wa Buluu. Vipaumbele vya Wizara ni pamoja na elimu na uwezeshaji, usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ya bahari, utafiti wa uvuvi na maliasili za bahari, ujenzi wa miundombinu ya uvuvi, mwani na mazao ya baharini, kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya baharini, upatikanaji wa masoko katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa Rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inategemea kutekeleza malengo yafuatayo kwa mujibu wa bajeti iliyowekwa:

i. Ununuzi wa Meli moja kubwa ya kisasa ya Uvuvi.

ii. Kukamilisha Upokeaji na Ugawaji kwa wananchi Boti 577 za Uvuvi, mabwawa 100 ya majongoo bahari, mabwawa 60 ya ufugaji wa kaa na mabwawa 40 ya ufugaji wa samaki.

iii. Kutoa elimu kwa wadau wa Sekta ya Uchumi wa Buluu wakiwemo wafaidika wa fedha za ahweni ya UVIKO19 kutoka IMF.

iv. Ujenzi wa bandari mbili za Uvuvi katika maeneo ya Kizimkazi Unguja bandari moja na bandari ya pili eneno la Shumba Pemba.

v. Ujenzi wa Kiwanda cha Kutengenezea Boti na ujenzi wa mtambo wa kusarifia samaki na mitambo ya baridi kupitia kampuni ya ZAFICO.

vi. Kuanza utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya baharí (Marine Spatial Plan).

vii. Kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira kwa kamati 91 za uvuvi Unguja na Pemba na kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini na ukulima wa mwani kibiashara.

viii. Kukamilisha Sheria ya mafuta na Gesi asilia pamoja na kuanza uhamasishaji wa matumizi ya sera na sheria hizo.

ix. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa Bohari ya Mafuta (Bulk Storage facilities) pamoja na miundombinu ya usambazaji wa mafuta.

x. Kuanza hatua za awali za Ujenzi wa Bohari ya Gesi (Natural Gas/LPG Storage Facility) pamoja na miundombinu ya usambazaji wa Gesi.

xi. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa kituo cha kuhifadhi taarifa za mafuta na Gesi Asilia (National Data Repository au NDR)

xii. Kukamilisha kuchukua taarifa kwa kiwango cha 3D na kuchimba kisima cha majaribio kupitia kampuni ya RAK-GAS.

xiii. Kufungua maeneo mapya kwa ajili ya kuwaalika wawekezaji waendelee na utafiti wa uendelezaji wa utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi Asilia Zanzibar.

xiv. Kuendeleza mashirikiano ya kikanda na Kimataifa katika kuleta maendeleo ya Uchumi wa Buluu ikiwemo maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini na vilevile Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU**

**66. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu imegawika katika programu ndogo moja nayo ni programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu. Aidha Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu ina huduma zake kuu mbili ambazo ni Uratibu wa Uchumi wa Buluu na Udhibiti wa Ufuatiliaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

**67. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu dhumuni lake kubwa ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 14,203,801,496.** Kati ya hizo **TZS 1,200,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS 228,501,496** ni kwa ajili ya Mishahara, na **TZS 1,775,300,000** ni RUZUKU kwa ZPRA. Matumizi ya fedha za Ruzuku za ZPRA ni kama ifuatavyo: **TZS 1,173,200,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; na **TZS 602,100,000** ni mishahara. Aidha Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imepatiwa **TZS 11,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu**

**Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu inalenga kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla.

**68. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Programu ndogo ya Uchumi wa Buluu kupitia huduma zake inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kufanya utafiti wa utambuzi wa hali halisi ya matumizi ya maeneo ya bahari;

ii. Kufanya uchambuzi wa kisera na muundo utakaosaidia mpango wa wa matumizi ya maeneo ya bahari; na

iii. Kufanya upangaji na uandishi wa mpango wa matumizi ya maeneo ya bahari.

iv. Kushajiisha shughuli za uratibu miongoni mwa sekta za kipaumbele za uchumi wa buluu;

v. Kuhamasisha na kujenga uwezo kwa jamii kuhusu Uchumi wa buluu;

vi. Kuandaa Mfuko wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;

vii. Kuratibu uwezeshaji, uongezaji thamani na kuimarisha masoko ya bidhaa za uchumi wa buluu;

viii. Kuratibu utafiti wa utambuzi wa mahitaji katika kuandaa na kusimamia 'Dashboard' ya uchumi wa buluu na 'Akaunti ya Satellite'; na

ix. Kuratibu ushiriki wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika shughuli za uchumi wa buluu.

**69. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 1,428,501,496** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo, **TZS 1,200,000,000** matumizi mengineyo na **TZS 228,501,496** Mishahara.

Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA)

**70. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inalenga kuendeleza

majukumu yake ya kusimamia na kudhibiti shughuli zote za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

**71. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia imepanga kutekeleza Majukumu yake kupitia vipaumbele vifuatavyo: -

1. Kuendelea kusimamia zoezi la Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya Mtetemo wa kina (3D) pamoja na RAKGas kwa upande wa kitalu cha Pemba – Zanzibar.

2. Kuendelea na matayarisho ya kazi ya ugawaji wa vitalu vipya vya Mafuta na Gesi Asilia katika Maeneo ya upande wa mashariki ya bahari.

3. Kuendeleza Programu ya kutoa uelewa kwa Jamii kuhusiana na masuala ya Mafuta na Gesi Asilia ambapo jumla ya programu 60 zitaendeshwa.

4. Kuendelea na kazi ya kuandaa Rasimu mbili (2) za Kanuni na Miongozo miwili (2) ya Kitaalamu ya kusimamia shughuli za Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

5. Kuimarisha na kuendeleza mfumo wa taarifa za wadau wanaohusika na shughuli za mafuta na gesi asilia, kusimamia taarifa za mafuta na gesi asilia pamoja na kutoa taarifa na machapisho kuhusu shughuli za Mafuta na Gesi Asilia.

6. Kuendelea kushirikiana na Wadau mbali mbali ikiwemo washirika wa Maendeleo katika kuimarisha na kutekeleza mipango ya mafunzo ya Mafuta na Gesi Asilia.

7. Kuimarisha mazingira ya kazi kwa watendaji ikiwemo ubora wa Ofisi, nguvu kazi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi waliopo ili kuleta ufanisi zaidi kwa Mamlaka.

**72. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inaombewa jumla ya **TZS 1,775,300,000** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **TZS 1,173,200,000** ni matumizi mengineyo na **TZS 602,100,000** Mishahara.

**Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar**

73. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inalenga kuendeleza utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa kampuni

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

    i. Kujenga mazingira bora ya kufanyia kazi kwa Wafanyakazi.

    ii. Kujenga uwezo kwa Watendaji wa Kampuni katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia;

    iii. Uendeshaji wa shughuli za Mkataba wa mgawanyo wa Mafuta na Gesi Asilia (PSA);

    iv. Ununuzi wa vifaa vya kuhifadhia taarifa za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwa Majiolojia pamoja na kuanzisha mfumo wa akiba wa kuhifadhi taarifa za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia;

    v. Kutoa uelewa wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi za Serikali na wananchi.

    vi. Kushiriki katika biashara ya mafuta na gesi kwa mkondo wa kati na chini kupitia Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

75. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inaombewa jumla ya **TZS 4.4 bilioni** kwa matumizi ya kawaida na Maendeleo.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI**

76. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari;

77. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 73,161,642,646.** Kati ya fedha hizo, **TZS 2,606,642,646** ni kwa kazi za kawaida ambapo **TZS 935,000,000** ni kwa matumizi mengineyo, **TZS 1,039,142,646** ni Mishahara na **TZS 632,500,000** ni RUZUKU. Katika kutekeleza miradi ya maendeleo programu hii inaombewa jumla ya **TZS 70,555,000,000.** Kati ya hizo **TZS 41,000,000,000** ni kutoka SMZ na **TZS 29,555,000,000** ni kutoka kwa Washirika wa maendeleo.

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji waMazao ya Baharini**

78. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu ndogo hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendelea kuimarisha kilimo cha mwani na kuongeza uzalishaji wa mwani kutoka tani 12,000 hadi tani 15,000 kwa kuwapatia elimu ya kisasa ya ukulima wa mwani pamoja na kuwapatia vifaa vya kulimia mwani vitakavyosaidia kuongeza uzalishaji.

ii. Kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo 5000 kuweza kuvua katika maji ya kina kirefu kwa kuwapatia zana pamoja na elimu itakayowawezesha kuvua katika maji ya kina kirefu.

iii. Kuendeleza miundombinu ya kisasa ya masoko na madiko ya samaki 6 (Unguja na Pemba).

iv. Kuendelea kutoa elimu ya ufugaji wa samaki, kaa na majongoo bahari kwa vikundi vya ufugaji 200 Unguja na Pemba.

v. Kuendeleza uzalishaji wa vifaranga vya samaki, kaa na majongoo bahari kuptia kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki (Hatchery).

vi. Kujenga mashamba mapya na kuyaendeleza mashamba ya mfano ya ufugaji wa majongoo bahari na Kaa Unguja na Pemba.

vii. Kuendelea kutoa elimu juu ya usimamizi wa ubora wa samaki na mazao mengine ya baharini ili kuongeza soko la ndani na la nje.

**79. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu ndogo hii inaombewa jumla ya **TZS 72,710,642,646** kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo, **TZS 484,000,000** ni kwa matumizi mengineyo, **TZS 1,039,142,646** ni kwa Mishahara; na RUZUKU ni **TZS 632,500,000** (**TZS 320,000,000** ni Ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi na Mazao ya Baharini na **TZS 312,500,000** ni Ruzuku kwa Kampuni ya Uvuvi ZAFICO). Katika kutekeleza miradi ya maendeleo programu hii ya Wizara inaombewa jumla ya **TZS 70,555,000,000.** Kati ya hizo, **TZS 41,000,000,000** ni kutoka SMZ na **TZS 29,555,000,000** ni kutoka kwa Washirika wa maendeleo.

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini**

**80. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kufanya tafiti 3 kwa mwaka 2022/23 zinazohusiana na Uvuvi, Mazingira ya baharini, na Mazao na Rasilimali za Baharini na kutowa mrejesho kwa jamii;

ii. Kuanzisha na kuimarisha maabara ya kisasa ya kuthaminisha mazao ya baharini yakiwemo Samaki na Mwani;

iii. Kuanzisha maabara ya tafiti za mifumo na mienendo ya Bahari (Oceanographic laboratory) kwa lengo la kuimarisha utoaji wa Taarifa kwa Wavuvi na matumizi ya Bahari;

iv. Kuanzisha Ofisi ndogo na kituo kidogo cha Utafiti Pemba;

v. Kuchapisha vitabu 500 vya Muongozo wa Ufugaji Majongoo Bahari kwa njia ya Kitaalamu na kuvisambaza kwa wadau;

vi. Kuajiri watafiti na wataalamu mbali mbali, na kuwajengea uwezo wafanyakazi 14 watakaotoa huduma bora katika kutekeleza tafiti za uvuvi na maliasili za baharini Zanzibar;

vii. Kuendeleza mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na maliasili za Baharini Zanzibar;

viii. Kuchapisha vitabu 500 vyenye tarifa fupi za tafiti za Uvuvi na Mazao ya Baharini zilizofanyika Zanzibar kuanzia mwaka 1999-2020 kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi;

ix. Kununua vifaa vya kisasa vitakavowezesha kufanyika kwa tafiti bora za uvuvi, rasilimali za Baharini, na mienendo na mifumo ya Bahari;

x. Kuanzisha Jarida la Tafiti za Uvuvi, Rasilimali za Baharini, na mienendo na mifumo ya Bahari;

xi. Kuandaa kitabu cha taarifa za Tafiti kwa Sera za Uchumi wa Buluu na Uvuvi (Policy Briefs for Blue Economy and Fisheries);

xii. Ununuzi wa vifaa vya Tehama, pamoja na vifaa vya kuhifadhia taarifa za tafiti za Uvuvi, mazao ya Baharini, rasilimali za Baharini, na mienendo na mifumo ya Bahari.

81. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini inaombewa jumla ya **TZS 320,000,000** kwa matumizi ya kawaida ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini.

**Kampuni ya Uvuvi Zanzibar - ZAFICO**

82. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) kwa Mwaka wa Fedha 2022-2023, inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuvua na kununuwa kwa wakala tani 120 za samaki na kuuza katika taasisi za Serikali, Kampuni, Hoteli na Wananchi.

ii. Kuanza ujenzi wa viwanda Mkokotoni Fungurefu ikiwemo cha utengenezaji wa Boti na Uchakataji na usarifu wa mazao ya baharini.

iii. Kuanza Ujenzi wa vyumba vya baridi (COLD ROOM) kwa ajili ya kuhifadhia samaki Malindi.

iv. Kuendeleza Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa Kama pamoja na chanja za kuanikia dagaa kwa wajasiriamali wa dagaa wa maeneo ya Bububu, Kama na Ngalawa.

v. Kuendelea na matayarisho ya Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Samaki Shumba Mjini kwa upande wa Pemba

vi. Kuendeleza Mradi wa Uuzaji wa Samaki

vii. Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa Uanzishwaji wa Kampuni ya Zanzibar Aquaculture Harvest Company (ZAHC).

viii. Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 1000 wa samaki na dagaa juu ya njia bora ya kuhifadhi bidhaa hizo Unguja na Pemba.

ix. Kutoa Mafunzo kwa wafanyakazi 10 wa Kampuni katika fani mbali mbali. Wafanyakazi 7 mafunzo ya muda mfupi na 3 muda mrefu.

x. Kuwapatia Mshine za boti wavuvi 250 Unguja na Pemba kupitia mkopo wa fedha kutoka AMANA bank.

**83. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO imeombewa **TZS 312,500,000** Ruzuku ya mishahara kutoka SMZ. Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaipatia ZAFICO jumla ya **TZS 11,000,000,000** kwa kutekeleza mradi wa kutengeza Maboti na kiwanda cha kusarifu samaki na Dagaa kwa ubia na kampuni ya HAIRU kutoka SRILANKA.

Aidha, kampuni ya ZAFICO inatarajia kupata **TZS 4.6 bilioni** ikiwa ni pato litakalotokana na biashara zake za ndani.

**Programu Ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari**

84. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

    i. Kutoa elimu ya Uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii na kuzijengea uwezo kamati za uvuvi 102 Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi na kusimamia rasilimali za bahari kwa kuanzisha maeneo ya ufungaji wa pweza na samaki wa miambani.

    ii. Kuimarisha Doria /Ulinzi shirikishi 336 katika maeneo ya Maji ya Ndani kwa kununua Boti 5 za Doria ili kudhibiti Uvuvi haramu.

    iii. Kuwawezesha jamii kuweka matumbawe Bandia katika maeneo ya Hifadhi za bahari ili kuongeza uzalishaji wa samaki

    iv. Kuongeza maeneo mapya ya hifadhi shirikishi.

    v. Kufanya ufuatiliaji katika maeneo ya miamba na mazalio ya samaki.

    vi. Kufanya usafi wa fukwe na mafungu.

    vii. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi kumi kuhusu usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ya bahari.

    viii. Kushirikiana na washirika wa kimaendeleo katika kuendeleza uhifadhi wa mazingira ya baharini.

85. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu hii ndogo ya Uhifadhi inaombewa **TZS 451,000,000** kwa matumizi mengineyo ya kazi za kawaida.

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

86. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi kwa ustawi kwa sekta.

**Programu imegawika katika programuu ndogo tatu nazo ni:**

i. Programu ya Utawala na Uendeshaji
ii. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti
iii. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba

87. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inaombewa jumla ya **TZS 2,296,955,858** kwa kazi za kawaida kati ya fedha hizo **TZS 1,162,155,858** mishahara, na **TZS 1,134,800,000** matumizi mengineyo.

**Programu ndogo ya utawala na uendeshaji**

88. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**Shabaha zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji kwa Mwaka 2022/2023**

i. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi 105.

ii. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 5 kwa mafunzo ya muda mrefu na 15 mafunzo ya muda mfupi.

iii. Ufuatiliaji na udhibiti wa Mali za Serikali.

iv. Kutengeneza Hifadhi Data ya Rasilimali Watu (Human Resource Data Base) pamoja na Tovuti ya Wizara.

v. Kutengeneza Mkataba wa Huduma kwa Wateja pamoja na Kutekeleza Upimaji wa Utendaji wa Wafanyakazi.

vi. Kuendelea kutoa taarifa za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia vyombo vya habari, majarida na njia ya mtandao na Kuandaa vipindi vya TV na redio.

89. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, inaombewa jumla ya **TZS 1,025,448,539** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **TZS 450,448,539** mishahara na **TZS 575,000,000** matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti**

90. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

**Shabaha zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti 2022/2023**

91. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuwasilisha Sheria za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Mafuta na Gesi) katika vikao vya Baraza la Wawakilishi na Baraza la Mapinduzi pamoja na kuanza matumizi ya Sera hizo.

ii. Kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Agenda ya Utafiti Zanzibar na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo.

iii. Kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika ukusanyaji na usambazaji wa takwimu.

iv. Kushirikiana na Tume ya Mipango katika Kuandaa miradi mipya ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na kuratibu usimamizi wa miradi inayoendelea ya Wizara **(Kiambatisho Nam 8A-F).**

v. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti na mpangokazi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na kuwasilisha utekelezaji kwa mujibu wa miongozo ya Baraza la Wawakilishi na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

vi. Kuratibu kazi za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

vii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini wa kazi za Wizara na miradi ya maendeleo.

viii. Kuratibu Mashirikiano ya Wizara za SMT na SMZ pamoja na mashirikiano ya ndani, kikanda na kimataifa.

**92. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango inaombewa jumla ya **TZS 574,317,420** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **TZS 134,517,420** ni mishahara, na **TZS 439,800,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba**

**93. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**94. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu vikao 4 na ziara za Kamati ya Uchumi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara Pemba.

ii. Kufanikisha ziara 10 za viongozi wa Wizara na Kitaifa.

iii. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, na taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Pemba.

iv. Kufanya vikao vya uendeshaji na usimamizi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana na Idara na taasisi mbali mbali mtambuka za Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Pemba.

v. Kuimarisha mashirikiano na taasisi nyenginezo za Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii.

95. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, Programu hii inaombewa jumla ya **TZS 697,189,899** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **TZS 577,189,899** ni mishahara na **TZS 120,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

96. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **TZS 2,259,412,000** kupitia vianzio vyake vinne vya Unguja na Pemba.

97. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 89,662,400,000.** Kati ya fedha hizo **TZS 8,101,400,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida ambapo **TZS 2,429,800,000** ni Mishahara, **TZS 3,263,800,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS 2,407,800,000** ni RUZUKU kutoka SMZ ambayo ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar. Kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Wizara imetengewa **TZS 81,555,000,000** ambapo **TZS 52,000,000,000** kutoka SMZ na **TZS 29,555,000,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**HITIMISHO**

98. **Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa nachukua nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano na Wizara yetu ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi katika utekelezaji wa programu na utoaji huduma mbali mbali za Uchumi wa Buluu ikiwemo sekta za Uvuvi, Ukulima wa Mwani, Ufugaji wa Mazao ya Baharini, Utafiti,

Uhifadhi wa Bahari, na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais (Ikulu); Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ikiwemo Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao wamekuwa karibu sana nasi katika kulipeleka mbele gurudumu letu la maendeleo ya Uchumi wa Buluu; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, ikiwemo pia wadau wetu wa karibu kabisa wa KMKM; Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji ikiwemo ZIPA; Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Wizara ya Afya; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**99. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia inatoa shukrani zake za dhati na za kipekee kwa wadau wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa mipango yake ya Uchumi wa Buluu. Taasisi hizi ni pamoja na Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano; Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT; Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT), ikiwemo Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania; Wizara ya Nishati SMT; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (SMT). Shukurani pekee ziwaendee Waheshimiwa Mabalozi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walio mstari wa mbele katika kuutangaza Uchumi wa Buluu duniani kote.

**100. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatoa shukrani pia kwa Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) na Jumuiya ya WIOMSA, TNC, WWF, WCS, Marine Cultures, Milele Foundation, Mwambao, katika utekelezaji wa programu za utafiti, uwezeshaji na uhifadhi wa bahari. Vilevile, nachukua fursa hii kwa kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa yanayoendelea kushirikiana na Wizara kwa hali na mali katika juhudi za kuendeleza utekelezaji wa mipango na mikakati yetu ya Uchumi wa Buluu. Hizi zikiwemo Japan, China, Korea Kusini, Norway,

Ireland, Ufaransa, Ujerumani, Uingereza, Canada, Marekani, Uholanzi, Umoja wa Falme za Kiarabu na Oman. Aidha, nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: UNDP, UN Women, UNEP, UNECA, Umoja wa Afrika, SADC, Jumuiya ya Afrika Mashariki, EU, USAID, Benki ya Dunia, IFAD, NORAD, FAO, WFP, SWIO-FC, JICA, KOICA, Tony Blair Institute, Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Jumuiya ya Nchi Zinazopakana na Bahari ya Hindi (IORA), Kamisheni ya Jodari ya Bahari ya Hindi (IOTC), n.k. kwa mashirikiano yao ya karibu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa ajenda ya Uchumi wa Buluu.

101. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani za pekee kwa wavuvi, wakulima wa mwani, wafugaji wa mazao ya baharini na wanakamati za hifadhi za uvuvi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuendeleza na kuimarisha uvuvi pamoja na uhifadhi wa rasilimali na ufugaji wa mazao ya baharini. Pia, napenda kumshukuru Katibu Mkuu na Afisa Mdhamini Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi za Wizara yangu pamoja na watumishi wote wa Wizara pasi na kuzisahau Manispaa, Mabaraza ya Mji na Halmashauri na wadau wote wa Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa Shabaha za Wizara kwa mwaka 2021/2022. Matarajio yetu kwamba tutaendelea kushirikiana tena katika mwaka 2022/2023.

102. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Ulinzi na Usalama, Baraza la Biashara la Taifa, Majukwaa ya Vijana, Vikosi vya SMZ na vyombo vya Habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu,

103. **Mheshimiwa Spika** na Waheshimiwa Wajumbe

nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.

.......................................................


MHE. SULEIMAN MASOUD MAKAME (MBM)

**WAZIRI, WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**


**ZANZIBAR.**

# VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho Nam. 1a: Uzalishaji wa Samaki (Tani)**



**Kiambatanisho Nam. 1b: Usafirishaji wa Mazao ya Baharini (Tani)**



**Kiambatanisho Nam. 2: Jadweli la Upatikanaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/22**

| Kasma | Maelezo | Makadirio ya Mapato 2021/22 | Mapato halisi Julai hadi Marchi 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Ofisi Kuu Pemba** | | | | |
| | Leseni Za Uvuvi | 59,066,726 | 17,431,500 | 29.5 |
| | Ada Mazao Baharini | 44,300,044 | 36,358,800 | 82.07 |
| | Tiketi za Wageni na Faini (PECCA) | 81,216,748 | 19,535,420 | 24.05 |
| **Jumla Ndogo** | | **184,583,517** | **73,325,720** | **39.72** |
| **Idara ya Uvuvi** | | | | |
| | Leseni Za Uvuvi | 236,266,902 | 37,294,500 | 15.78 |
| | Ada Mazao Baharini | 487,300,486 | 493,227,664 | 101.2 |
| | Tiketi za wageni faini  na dago ( MENAI na MIMCA) | 527,170,526 | 390,542,015 | 74.08 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,250,737,914** | **921,064,179** | **73.64** |
| Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu | Mapato Ya Uvuvi Wa Bahari Kuu | 1,289,890,000 | 238,892,788 | 18.52 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,289,890,000** | **238,892,788** | **18.52** |
| **JUMLA KUU** | | **2,259,412,000** | **1,233,282,687** | **54.6** |

**Kiambatanisho Nam. 3: Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2021- Machi 2022**

| PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | Fedha Iliyopatikana Kwa Kipindi Cha Julai-Machi 2021-2022 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mshahara | Matumizi ya Kawaida | Ruzuku Kawaida | Ruzuku Mishahara | Maendeleo SMZ | Maendeleo Mhisani | Jumla |
| **PL0201 Maendeleo ya Uchumi wa Buluu** | | **233,774,986** | **340,000,000** | **449,720,870** | | | **1,023,495,856** |
| **SL020101**Uratibu wa Uchumi wa Buluu | | 233,774,986 | | | | | 233,774,986 |
| Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia(ZPRA) | | | 340,000,000 | 449,720,870 | | | 789,720,870 |
| **PL0104 Maendeleo ya Uvuvi** | **842,387,115** | **512,233,621** | **72,544,000** | **145,432,860** | **32,360,949,614** | **2,435,426,023** | **36,368,973,233** |
| **SL010401** Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya bararini | 842,387,115 | 106,915,651 | | | 32,360,949,614 | 2,435,426,023 | 35,745,678,403 |
| SL010402 Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari | | 80,427,542 | | | | | 80,427,552 |
| SL010402 Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Bahari | | | 72,544,000 | | | | 72,544,000 |
| Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) | | 324,890,428 | | 145,432,860 | | | 470,323,288 |
| PL0105 Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 927,786,895 | 356,881,821 | | | | | 1,284,668,716 |
| SL010501 Utawala na Uendeshaji wa kazi za Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 423,986,255 | 238,328,519 | | | | | 662,314,774 |
| SL010502 Mipango, Sera na Ufatifi wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 84,542,125 | 92,866,562 | | | | | 177,408,687 |
| SL010502 Uratibu Ofisi Kuu Pemba | 419,258,515 | 25,686,740 | | | | | 444,945,255 |
| Jumla Kuu | 1,770,174,010 | 1,102,890,428 | 446,742,304 | 595,153,730 | 64,721,899,228 | 4,870,852,046 | 38,677,137,805 |

Kiambatanisho Nam. 4: Jadweli la Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo Julai 2021 hadi Machi 2022

| S/N | MRADI | MAKISIO 2021/2022 | | | FEDHA ZILOPATIKANA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | SMZ | MUHISANI | JUMLA | SMZ | MUHISANI | JUMLA |
| 1. | Mradi wa usimamizi wa shughuli za uvuvi wa kanda ya kusini mashariki mwa bahari ya hindi (swiofish) | | 4,443,487,000 | 4,443,487,000 | | 2,435,426,023 | 2,435,426,023 |
| 2. | Mradi wa Ujenzi wa Soko la Malindi | 3,600,000,000 | 21,141,600,000 | 24,741,600,000 | 2,333,609,614 | | 2,333,609,614 |
| 3. | Mradi wa ahuweni wa UVIKO 19 ukiwemo Ujenzi wa maboti 28,845,440,000 bilioni, Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa 486,900,000 milioni, Mafunzo kwa wadau 695,000,000 milioni | | | | | 30,027,340,000 | 30,027,340,000 |
| 4. | Mradi wa kuanzisha mashamba ya kufuga samaki | - | - | - | - | - | - |
| 5. | Mradi wa ujenzi wa kituo cha usarifu na uhifadhi wa bidhaa za samaki | - | - | - | - | - | - |
| | Jumla | 3,600,000,000 | 25,748,235,000 | 29,185,087,000 | 2,333,609,614 | 32,462,766,023 | 34,796,375,637 |

**Kiambatanisho Nam. 5: Jadweli la Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka 2022/ 2023**

| KASMA | MAELEZO | MAKADIRIO YA MAPATO 2022/23 |
|---|---|---|
| AFISI KUU PEMBA | Leseni za Uvuvi na Chombo anachovulia | 11,814,000 |
| | Ada Mazao Baharini | 132,640,000 |
| | Tiketi za Wageni na Faini ( PECCA) | 81,216,000 |
| Jumla Ndogo | | 225, 670,000 |
| IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI | Leseni ya Uvuvi na Chombo anachovulia | 17,720,000 |
| | Ada ya Usafirishaji wa Mazao ya Baharini | 198,961,000 |
| | Tiketi za Wageni Faini na Dago ( Menai, Mimca) | 527,171,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **743,852,000** |
| MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU | Uvuvi wa bahari kuu | 1,289,890,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,289,890,000** |
| **JUMLA KUU** | | **2,259,412,000** |

**Kiambatanisho Nam. 6: Jadweli la Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Kazi za Kawaida kwa Mwaka 2022/2023**

| PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | MAKADIRIO YA FEDHA ZA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2022/2023 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MSHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU KAWAIDA | RUZUKU MISHAHARA | MAENDELEO SMZ | MAENDELEO MHISANI | JUMLA |
| **PL0201** Maendeleo ya uchumi wa buluu | 228,501,496 | 1,200,000,000 | 1,173,200,000 | 602,100,000 | 11,000,000,000 | | 14,203,801,496 |
| **SL020101** Maendeleo ya Uchumi wa Buluu | 228,501,496 | 1,200,000,000 | | | | | 1,428,501,496 |
| Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia(ZPRA) | | | 1,173,200,000 | 602,100,000 | 5,000,000,000 | | 6,775,300,000 |
| Kampuni ya mafuta na gesi asilia (ZPDC) | | | | | 6,000,000,000 | | 6,000,000,000 |
| **PL0202** Maendeleo ya Uvuvi | 1,039,142,646 | 935,000,000 | 320,000,000 | 312,500,000 | 41,000,000,000 | 29,555,000,000 | 73,161,642,646 |
| **SL020201** Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa mazao ya Bahari | 1,039,142,646 | 484,000,000 | | | 30,000,000,000 | 29,555,000,000 | 61,078,142,646 |
| Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Bahari | | | 320,000,000 | | | | 320,000,000 |
| Kampuni ya uvuvi Zanzibar (ZAFICO) | | | | 312,500,000 | 11,000,000,000 | | 11,312,500,000 |
| **SL020202** Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari | | 451,000,000 | | | | | 451,000,000 |
| **PLO203** Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 1,162,155,858 | 1,134,800,000 | | | | | 2,296,955,858 |
| **SL020301** Utawala na Uendeshaji | 450,448,539 | 575,000,000 | | | | | 1,025,448,539 |
| **SL020302** Mipango Sera na Utafiti | 134,517,420 | 439,800,000 | | | | | 574,317,420 |
| **SL020303** Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba | 577,189,899 | 120,000,000 | | | | | 697,189,899 |
| **Jumla Kuu** | **2,429,800,000** | **3,269,800,000** | **1,493,200,000** | **914,600,000** | **52,000,000,000** | **29,555,000,000** | **89,662,400,000** |

**KIAMBATANISHO NAM. 7: MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023**

| MRADI | MAKISIO 2022/2023 | | |
|---|---|---|---|
| | **MUHISANI** | **FEDHA ZA MRADI** | **JUMLA - TZS** |
| Mradi wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu i. (Tanzania Scaling Up Sustainable Fisheries and Aquaculture Management) | BENKI YA DUNIA | 13,455,000,000 | 13,455,000,000 |
| Mradi wa kuendeleza Kilimo na Uvuvi (Agriculture and Fisheries Development programme) | IFAD | 13,800,000,000 | 13,800,000,000 |
| Mradi jumuishi wa uwezeshaji wa wanawake katika ufugaji wa mazao ya baharini (Women Empowerment in Integrated Mari-culture Value Chains in Zanzibar) | KOICA | 2,300,000,000 | 2,300,000,000 |
| Mradi wa Ujenzi wa bandari 2 za kisasa (Integrated Fish Port, Landing Sites and Market Facility) | SMZ | 30,000,000,000 | 30,000,000,000 |
| Mradi wa uanzishwaji wa Viwanda vya maboti na kusarifu samaki na dagaa | SMZ | 11,000,000,000 | 11,000,000,000 |
| Kuanzisha kituo cha kuhifadhi taarifa za mafuta na Gesi Asilia (National Data Repository au NDR | SMZ | 5,000,000,000 | 5,000,000,000 |
| Ujenzi wa Bohari ya Gesi (Natural Gas/LPG Storage Facility) pamoja na miundombinu ya usambazaji wa Gesi | SMZ | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 |
| Ujenzi wa Bohari ya Mafuta (Bulk Storage facilities) pamoja na miundombinu ya usambazaji wa mafuta | SMZ | 4,000,000,000 | 4,000,000,000 |
| **JUMLA** | | | **81,555,000,000** |

**Kiambatanisho Nam. 8A: Usimamizi wa shughuli za Uvuvi wa kanda ya Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi (SWIOfish)**

| |
|---|
| Gharama za mradi: Kwa mwaka 2021/2022 Mradi uliombewa TZS 4,443,487,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo (Benki ya Dunia). Hadi kufikia Machi, 2022 mradi ulipatiwa TZS 2,435,426,023 kutoka kwa washirika wa maendeleo na hakuna fedha zilizopatikana kutoka SMZ |
| Lengo Kuu la mradi: Kuimarisha usimamaizi wa shughuli za uvuvi |
| Malengo ya mwaka: 2021/2022<br>Kutoa taaluma na Usimamizi wa uvuvi wa kipaumbele<br>Kukamilisha utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Uvuvi na mapitio ya taratibu za sheria ya Uvuvi numb 7, 2010<br>Kuendelea kuwalipia wanafunzi 5 MSc na 2 PhD katika mafunzo yao ya uvuvi na Kuendelea na tafiti katika maeneo husika<br>Kufuatilia uchukuwaji wa taakwimu sahihi na Kufanya mikutano ya mrejesho wa wadau (Jamii)<br>Kukamilisha Mipango ya usimamizi wa uvuvi uliopewa kipaumbe (Pweza, Samaki wa kwenye Matumbawe, Jamii ya madagaa na Jamii ya jodari) kwa kuthibitishwa.<br>Kukamilisha na kuthibitisha mapitio na matayarisho ya Mipango ya Usimamizi wa maeneo ya hifadhi (GMPs) ikiwemo 3 ni mapitio na 2 mpya, Kuendelea na Mfunzao kwa jamii na kuthibitishwa kwa Taratibu za ushirikishaji wa jamii katika shughuli za usimamizi<br>Kuendelea kufanya doria katika katika maeneo ya hifadhi<br>Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 10 Kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya taasisi ya tafiti za uvuvi na Kununua na kuweka maboya katika maeneo ya hifadhi.<br>Kuendela na kuhamasisha na kupatiwa mafunzo ya kuweka na kukopa kwa ajili ya biashara inayohusiana na shughuli za uvuvi.<br>Kutekeleza shughuli za Ufuatiliaji na Tathminiza Mradi |
| UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MRADI WA SWIOfish<br>Mradi umekamilisha ripoti ya utafiti wa sekta ya uvuvi (Fisheries Enterprises Survey).<br>Kukamilika kwa Utafiti juu ya Value chain Analysis ya uvuvi uliopewa kipaumbele (Small pelagic, Reef Fisheries, Tuna and |

Tuna like Fisheries, Octopus and shrip).

Kukamilika kwa mipango mikuu 3 ya usimamizi wa uvuvi (samaki wa miamba, pweza na samaki wadogo wadogo).

Mradi upo katika hatua za mwisho za kukamilisha utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Sekta ya Uvuvi Zanzibar (Fisheries Master Plan) ambao tayari umewasilishwa katika kikao cha makatibu Waku una kupatiwa maoni.

Tafiti tano (Utafiti wa pweza, samaki wa miamba, samaki wadogo wadogo "small pellagics" pamoja na jodari na jamii ya samaki inayofanana nao zinaendelea

- Wanafunzi watano (5) wa shahada ya pili wamekamilisha masomo yao (Course work) na hivi sasa wanaendelea na tafiti zao.

Wanafunzi wanne (4) wa shahada ya pili tayari wamekamilisha masomo yao na kuripoti kazi. Aidha, wanafunzi 2 wa udaktari (PhD) wanaendelea na tafiti zao.

Kazi ya kufanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi nambari 7 ya mwaka 2010 inaendelea ambapo tayari rasimu ya awali ya sheria hiyo imetayarishwa. Aidha, vikao mbali mbali vya wadau wa sekta ya uvuvi vimefanyika kwa lengo la kukusanya maoni ili kuweza kupata sheria iliyobora itakayosimamia uvuvi endelevu hapa nchini.

Mradi upo katika hatua za kukamilisha kazi ya kufanya mapitio ya sera ya uvuvi ambapo Vikao vya kupitia rasimu hiyo vimefanyika Unguja na Pemba vilivyo washirikisha watumiaji wa rasilimali za bahari, taasisi za kiserikali na taasisi binafsi.

Rasimu za mwisho za mipango ya usimamizi ya maeneo ya hifadhi ya MIMCA, MENAI na PECCA pamoja na TUMCA na CHABAMCA pamoja na mipango mkakati ya doria za baharini (Monitoring Control and surveillance strateges) imewasilishwa na kupatiwa maoni. Hivi sasa Mshauri elekezi anaendelea na kazi ya kukamilisha mipango hiyo.

Kikao cha kukusanya maoni ya wadau wa sekta ya uvuvi kwa lengo la kuimarisha na kukamilisha mipango ya usimamizi ya maeneo ya hifadhi za bahari Unguja na Pemba.

Mradi umekamilisha ujenzi wa jengo la utafiti wa uvuvi na Mazao ya baharini (Marine Research Unit) na tayari jengo hilo limeanza kutumika. Jengo hili limezinduliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussen Ali Mwinyi.

Hivi sasa mradi upo katika hatua za kukamilisha ununuzi wa vifaa vya maabara kwa ajili ya taasisi ya utafiti wa uvuvi.

Ujenzi wa Afisi Mpya za hifadhi za baharí za TUMCA na CHABAMCA pamoja na kituo kipya cha doria za baharini Pungume umekamilika na tayari zimeanza kazi. Katika kuendeleza na kusimamia maeneo ya hifadhi za Bahari, Mradi umefanya

ukarabati wa majengo ya Ofisi za maeneo ya hifadhi za jamii huko PECCA, MIMCA, MBCA, Kikungwi pamoja na Misali.

Kazi ya kuandaa Mchoro pamoja na ripoti kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi ya kampuni ya ZAFICO kupitia kampuni ya Inros-Lackners ya Ujerumani ilikamilika.

Aidha, ripoti ya mwisho ya Kimazingira (EIA) pia iliyofanywa na Inros-Lackners ilikamilika na kupatiwa cheti na Mamlaka inayohusiana na usimamizi wa mazingira nchini kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo wa chelezo kwa ajili ya meli za ZAFICO.

Kazi ya kuyafanyia ukarabati soko la samaki la Nungwi imekamilika na tayari limekabidhiwa kwa wanachi na linaendelea na kazi.

Kwa upande wa Soko la Tumbe bado halijakabidhiwa kutokana na wananchi kuomba kazi ya ziada ambayo ombi lao linafanyiwa kazi

Kazi ya kuandaa mfumo wa taarifa za uvuvi (Fisheries Information System) imekamilika na tayari taarifa za uvuvi zimeanza kuingizwa katika mfumo huo.

**KIAMBATANISHO NAM. 8B: MRADI WA UJENZI WA SOKO LA SAMAKI MALINDI**

| |
|---|
| Gharama za mradi: Kwa mwaka 2021/2022 Mradi uliombewa **TSH. 3,600,000,000** kutoka SMZ na **TSH. 21,141,600,000** kutoka washirika wa maendeleo (JICA) zimetengwa kutekeleza mradi huu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi, 2022 mradi ulipatiwa **TZS. 2,333,609,614** kutoka kwa washirika wa maendeleo na hakuna fedha zilizopatikana kutoka SMZ |
| **Lengo Kuu la mradi:** Kuwawezesha wadau wanaotumia diko la Malindi kuuza na kununua samaki wao wakiwa salama kiafya pamoja na kuwepo mazingira mazuri ya kuweka vyombo vya uvuvi na biashara kwa wavuvi, wachuuzi, madalali, wauzaji wadogo wadogo na wanunuzi |
| **Malengo ya mwaka: 2021/2022**<br>• Kuendelea Ujenzi wa Lot 1 kwa<br>– Kumalizia ujenzi wa eneo la kuegesha vyombo vikubwa kwa kwa kuweka vifaa vya kufungia vyombo (Fender) na kusafisha eneo kwa kuondoa pile za muda na mchanga<br>– Kukamilisha ujenzi wa mashimo ya maji machafu (septic tanks)<br>– Kujenga jengo la kufanyia biashara na ofisi za uendeshaji<br>– Kukamilisha kutayarisha mipango ya uendeshaji (Fedha na Kanuni)<br>• Kuanza ujenzi wa Lot 2 kwa kufanya mambo yafuatayo.<br>– Kukarabati wa soko la zamani,<br>– Kujenga vyoo, Sehemu ya kuhifadhia genereta na Kibanda cha mlinzi,<br>– Sakafu ya nje, mitaro ya maji machafu na maeneo ya kuegeshea vyombo vya juu<br>• **Majukumu mengine ya SMZ**<br>– Kufanya ufuatiliaji wa hali ya kimazingira (Environmental Monitoring) katika eneo la ujenzi |

- Kufanya ufuatiliaji wa mambo ya kale (Archaeological survey) katika eneo la ujenzi
- Kuweka Mtambo wabarafu chenga na Jenereta
- Kufanya manunuzi wa vifaa vya samani
- Kufanya manunuzi na uwekaji wa viyoyozi ndani ya soko jipya
- Kufanya manunuzi ya vifaa vya vyengine vya soko (Boksi za Samaki, Majokofu, pampu ya kusafishia, Matangi ya maji, vibao vya kuchakatia Samaki, meza za kuhamisha,

**Utekelezaji wa Malengo**

**Ujenzi umefikia 70% kwa: Lot 1 60% na Lot 2 83%**

- Kukamilika kwa 100% ujenzi wa eneo la kuegeshea vyombo - Lot 1
- Ujenzi wa jengo la ofisi na biashara kwa 40% (kukamilisha mashimo ya maji taka, matofali na kukamilika kwa kuweka zege ghorofa ya kwanza) - Lot 1
- Kukamilika kwa ujenzi wa msingi wa jengo la biashara na ofisi (100%)
- Kumalizia sakafu ya ghorofa ya kwanza kwa kuweka zenge (98%)
- Kuanza kwa ukarabati (demolish) wa soko la zamani - Lot 2
- Kubomoa maeneo yaliyoharibika (100%)
- Kukamilika kwa kuezeka paa (100%)
- Kuanza kazi za plasta ya ndani (80%)
- Kukamilika kwa mpango wa usimamizi (Management guide) – Lot 1
- Ununuzi wa mtambo barafu (100%)
- Kukamilisha kwa 100% uwekaji wa miundombinu ya maji na umeme

**KAMBATANISHO NAM. 8C: MRADI WA UJENZI WA KIWANDA CHA KUSARIFU DAGAA**

Gharama za mradi: Kwa mwaka 2021/2022 Mradi uliombewa **TZS 4,277,607,000** kutoka katika fedha za maendeleo za SMZ kutekeleza mradi huu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi, 2022 mradi ulipatiwa **TZS.7.9** Bilioni kutoka kwa kutoka SMZ

**Lengo Kuu la mradi**: Kujenga kiwanda cha kusarifu Dagaa maeneo ya Mkokotoni Fungu Refu

**Malengo ya mwaka: 2021/2022**

1) Kutangaza zabuni kwa ajili ya kutafuta Mkandarasi wa ujenzi wa kiwanda
2) Kuaza ujezi wa kiwanda kwa hatua za awali
3) Kutafuta hati miliki ya eneo

**Utekelezaji wa Malengo**

- Kupatikana kwa eneo na kupimwa
- Kufanyika kwa tathmini ya kimazingira na kukamilika kwa ripoti hiyo.
- Kusaini mkataba na mzabuni wa majiko ambayo yatatumika kuchemshia dagaa
- Mkandarasi wa utengenezaji wa Chanja yupo katika eneo la mradi na kazi ya utengenezaji wa chanja imeshaanza.
- Kufunga mkataba na wazabuni wa ununuzi wa gari kwa ajili ya matumizi ya mradi
- Kukamilika kwa michoro ya ujenzi eneo la mradi.
- Kutoa zabuni ya ujenzi wa majengo ya miradi katika eneo la Kama.

**KIAMBATANISHO NAM. 8D: MRADI WA KUANZISHA MASHAMBA NA KUFUGA SAMAKI**

| |
|---|
| Gharama za mradi: **Kwa mwaka 2021/2022** Mradi uliombewa **TSH 463,800,000** kutoka katika fedha za maendeleo za **SMZ** kutekeleza mradi huu kwa kipindi cha mwaka wa fedha **2021/2022.** Hadi kufikia Machi, 2022 mradi haukapatiwa Fedha. |
| **Lengo Kuu la mradi:** Kuanzisha maabara ya kutotolea vifaranga vya samaki na kufuga katika mashamba yatakayojengwa baharini karibu na kisiwa cha Popo |
| **Malengo ya mwaka: 2021/2022**<br>1) Kulipa fidia za mazao kwenye shamba linalotarajiwa kujengwa kiwanda<br>2) Kutafuta hati miliki ya eneo linalotaka kujengwa kiwanda<br>3) Kuratibu shughuli zote za uanzishwaji wa kiwanda<br>4) Kutafuta Mshauri elekezi kwa ajili ya michoro ya kiwanda<br>5) Kuanza ujenzi wa kiwanda. |
| Kazi inayoendelea ni kufanya tathmini ya mazao kwa wananchi watakaoathirika na mradi kwa eneo la Bwereu<br>Hati Miliki imeshapatikana na kukabidhiwa kwa ZAFICO<br>Kazi za Uratibu zinaendelea zikiwemo:<br>• Zoezi la kufanya tathmini ya Kimazingira na Kijamii (Environmental and Social Impact assessment) linaendelea katika eneo la mradi Bwereu.<br>• Hati ya makubaliano ya Kampuni mpya ya pamoja (Zanzibar Aquaculture Harvest Company” (ZAHC) eneo la Bwereu. |

**KIAMBATANISHO NAM. 8E: MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA USARIFU WA BIDHAA ZA SAMAKI ZAFICO**

| |
|---|
| Gharama za mradi: Kwa mwaka 2021/2022 Mradi uliombewa **TSH 8,292,193,000** kutoka katika fedha za maendeleo za SMZ kutekeleza mradi huu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Hadi kufikia Machi, 2022 mradi haukupatiwa Fedha |
| Lengo Kuu la mradi:<br>Kuanzisha maabara ya kutotolea vifaranga vya samaki na kufuga katika mashamba yatakayojengwa baharini karibu na kisiwa cha Popo |
| Malengo ya mwaka: 2021/2022<br>1) Kuangusha jengo liliopo katika eneo kwa sasa<br>2) Kutangaza zabuni ya ujenzi wa kiwanda<br>3) Kuanza kwa ujenzi wa Kiwanda |
| Jengo halitoangushwa bali Kampuni mpya iliyoanzishwa itafanya marekebisho ya jengo hilo.<br>4) Makubaliano ya uwekezaji kati ya Kampuni ya ZAFICO na HAIRU kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa Ofisi na Vyumba baridi (cold Storage) Malindi yamekamilika.<br>5) Hatua inayofuata ni uwekaji na saini katika mikataba ya makubaliano hayo na kuanza utekelezaji.<br>6) Mradi huo utatekelezwa kwa njia ya Joint venture kati ya Kampuni ya HAIRU NAVAL CRAFT ENGENNERING COMPANY na ZAFICO.<br>7) Hatua zote za kutafuta visa za wataalamu kutoka kwenye Kampuni ya Hairu zimekamilika na matarajio kufika nchini hivi karibuni.<br>Ujenzi Utatekelezwa kwa pamoja kati ya ZAFICO na Kampuni ya HAIRU makubaliano yamekamilika. |

**KIAMBATISHO NAM 8F: MRADI WA KUIMARISHA UVUVI NA KILIMO (IFAD)**

| |
|---|
| Gharama za mradi: Kwa mwaka 2021/2022 Mradi ulikuwa katika hatua za matayarisho na hayakuombewa pesa kwenye bajeti. Mradi huu, unatarajiwa kutekelezwa na washirika wa maendeleo IFAD. |
| Lengo Kuu la mradi: ni "kuongeza tija endelevu, uthabiti, faida na biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki", kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. |
| Malengo ya mwaka: 2021/2022<br>• Kuanzisha uvuvi wa ubia na sekta binafsi kwa kununua meli 2 za uvuvi, kutayarisha mfumo wa uvuvi wa kibiashara, kutayarisha mfumo wa ubia na uchambuzi yakinifu wa uendeshaji<br>• Kufanya upembuzi wa kimazingira kwa meli za uvuvi wa maji ya kina kirefu, viwanda vya usarifu na chumba cha baridi<br>• Kutoa elimu na kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa kutayarisha nyaraka za kufundishia juu ya mbinu mpya za ukulima wa mwani, kuongeza thamani na mikutano mbalimbali, kufanya mikutano na kuwawezesha wakulima wa mwani kuongeza thamani pamoja na kufanya upembuzi wa shughuli za kilimo cha mwani na ufugaji wa Samaki katika maeneo ya hifadhi<br>• Kuwezesha ukulima wa mwani na wafugaji wa samaki kwa kuwapa vifaa na utaalamu ikiwemo kuanzisha vitalu vya tissue culture na mashamba darasa na kuwajengea uwezo pamoja na kuwawezesha kutayarisha vitalu vya mwani<br>• Kupunguza kupotea kwa ubora wa mazao (Samaki na mwani) kwa kujenga mtambo wa barafu na uendeshaji wake<br>• Kukuza usarifu wa mazao kwa kujenga makaushiyo ya jua na kununua makaushio ya umeme kwa dagaa, |

| |
|---|
| kununua mtambo wa kusarifu mwani, kunua magari ya kusafirishia Samaki<br>• Kuanzisha ufugaji wa mashamba darasa ya Samaki Unguja na Pemba<br>• Kuanzisha na kuendeleza makongamano ya kijinsia na lishe ikiwemo kutoa elimu ya lishe na uhamasishaji<br>Kuratibu shughuli za utekelezaji kwa kuendesha mikutano, kununua vyombo vya usafiri, Ufuatiliaji na tathmini, kufanya uchambuzi wa awali, na matumizi ya kuendeshea ofisi ya kawaida |
| Utekelezaji wa Malengo<br>SMT na SMZ zinafanya kazi na mshauri muelekezi kufanya Kazi hiyo. Aidha, Specification za meli zimeidhinishwa. Hata hivyo Zanzibar imekusudia kununua meli kubwa ya mita 26 badala ya Meli ndogo ya mita 18.<br>• Tangazo la kazi limetolewa na “shortlisting” imefanyika na kuwasilisha IFAD.Aidha interview kwa task force imefanyika na ripoti kamili kuwasilishwa IFAD<br>• “General Procurement Notice” ya mradi imetayarishwa na kutangazwa kwenye magazeti pamoja na kuandaliwa mpango kazi wa mradi.<br>• Kutambuliwa kwa Eneo la Ujenzi (Malindi), hadidu rejea za EIA na Michoro imetayarishwa.<br>• Kufanyika kwa matayarisho ya tathmini ndogo za mazingira kwa ujenzi wa viwanda<br>• Kutambuliwa kwa maeneo ya ujenzi wa Fisheries “training canters” Unguja na Pemba |
| Gharama kwa mwaka 2022/2023. Mradi unaombewa TZS. 13,800,000,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo (Benki ya Dunia) |

Malengo kwa mwaka 2022/2023

- Kuanzisha uvuvi wa ubia na sekta binafsi kwa kununua meli 2 za uvuvi, kutayarisha mfumo wa uvuvi wa kibiashara, kutayarisha mfumo wa ubia na uchambuzi yakinifu wa uendeshaji
- Ujenzi wa kiwanda jumuishi cha uchakataji wa samaki pamoja na mitambo baridi ya kuhifadhia samaki
- Ujenzi wa kiwanda jumuishi cha utengenezaji wa chakula cha samaki na mifugo mengine.
- Kusaidia miundombinu ya vituo vya mafunzo ya Uvuvi na Ufugaji wa viumbe bahari.
- Ujenzi wa kituo cha kupokelea na kulelea vifaranga
- Kuanzisha mashamba darasa ya ufugaji wa samaki ili kuhamasisha mifumo ya ufugaji wa viumbe bahari (kwa kutumia mabwawa na matangi) pamoja na kuanzisha karakana kwa ajili ya matengenezo ya vifaa na mitambo.
- Kujenga uwezo wa jamii katika kuendeleza uzalishaji wa mbegu bora za mwani.
- Ununuzi na uendeshaji wa meli yenye vifaa kamili vya uvuvi.
- Ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa barafu.
- Ununuzi wa Lori la Jokofu la tani 10.
- Ujenzi wa mtambo wa kukaushia mwani na dagaa unaotumia nguvu za jua.
- Ujenzi wa maabara na kitalu cha uzalishaji wa mbegu borta za mwani (tissue culture lab and nursery)
- Kufanya utafiti wa uzalishaji na ukuzaji wa aina tatu za samaki (majongoo bahari, kaa na milk fish).
- Kuandaa Mpango wa Biashara ya Uvuvi

**KIAMBATISHO NAM 8G: MRADI WA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU (SCALING UP BLUE ECONOMY)**

| **JINA LA MRADI** | **MRADI WA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU** |
|---|---|
| **MUDA** | **2022-2027** |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 89,700,000,000** |
| LENGO KUU | Kuendeleza uvuvi na ufugaji wa kwa kwa maendeleo ya uchumi wa buluu |
| FEDHA ZILIZOTEGWA KWA AJILI YA MRADI MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | Jumla ya **TZS 13,400,000,000** zimetengwa kutoka kwa washirika wa maendeleo (World Bank) |
| Malengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023:<br>1) Usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari.<br>2) Kuimarisha mfumo wa taarifa za pwani na bahari pamoja na ununuzi wa vifaa vya mawasiliano<br>3) Ujenzi wa majengo ya uhifadhi na utafiti.<br>4) Kuandaa na kupitia Sera, sheria na kanuni | |

**KIAMBATISHO NAM 8H: MRADI WA UWEZESHAJI WA WANAWAKE KATIKA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI**

| **JINA LAMRADI** | **MRADI JUMUISHI WA UWEZESHAJI WA WANAWAKE KATIKA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI** |
|---|---|
| MUDA | 2022-2027 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 12,650,000,000** |
| LENGO KUU | Kuwawezesha wakulima na wasindikaji wa mazao ya baharini ili kufikia maendeleo endelevu ya mnyororo wa thamani |
| FEDHA ZILIZOTEGWA KWA AJILI YA MRADI MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | Jumla ya **TZS 2,300,000,000** zimetengwa kutoka KOICA |
| Malengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023:<br>1) Kuanzisha mashamba nane ya majaribio ya mwani/majongoo bahari.<br>2) Kuanzisha vitalu vinne vya mwani na majongoo bahari<br>3) Kutoa mafunzo kwa wanwake 8000 wakulima wa majongoo bahari<br>4) Kutoaji wa vifaa kwa wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini<br>5) Usimamizi na uratibu wa mradi | |

**KIAMBATISHO NAM 8I: MRADI WA UJENZI WA BANDARI 2 ZA KISASA (INTEGRATED FISH PORT, LANDING SITES AND MARKET FACILITY)**

| **JINA LAMRADI** | **MRADI WA UJENZI WA BANDARI MBILI (2) ZA KISASA ENEO LA SHUMBA PEMBA NA KIZIMKAZI UNGUJA** |
|---|---|
| MUDA | 2022-2023 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 30,000,000,000** |
| 1) LENGO KUU | Kuwawezesha wavuvi kuweza kupata huduma za msingi za bandari na masoko |
| FEDHA ZILIZOTEGWA KWA AJILI YA MRADI MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | Jumla ya **TZS 30,000,000,000** zimetengwa kutoka kutoka katika fedha za maendeleo za SMZ |
| Malengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023:<br>1) Upembuzi yakinifu<br>2) Kuandaa mkutano wa zabuni<br>3) Kuandaa na kusimamia kazi za ujenzi | |

**KIAMBATISHO NAM 8J: MRADI WA UANZISHWAJI WA VIWANDA VYA MABOTI NA KUSARIFU SAMAKI NA DAGAA**

| **JINA LAMRADI** | **MRADI WA UANZISHWAJI WA VIWANDA VYA MABOTI NA KUSARIFU SAMAKI NA DAGAA** |
|---|---|
| MUDA | 2022-2024 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 50,000,000,000** |
| 2) LENGO KUU | Kuongeza ubora wa samaki na bidhaa za samaki na kupunguza upotevu wa ubora wa bidhaa |
| FEDHA ZILIZOTEGWA KWA AJILI YA MRADI MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | Jumla ya **TZS 11,000,000,000** zimetengwa kutoka kutoka katika fedha za maendeleo za SMZ |
| Malengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023:<br>1) Ujenzi wa kiwanda cha maboti<br>2) Uanzishwaji wa kiwanda cha teknologia ya chakula<br>3) Ujenzi wa sekta ya uvuvi n biashara | |

**KIAMBATISHO NAM 8K: MRADI WA KUANZISHA KITUO CHA KUHIFADHI TAARIFA ZA MAFUTA NA GESI ASILIA**

| **JINA LAMRADI** | **MRADI WA KUANZISHA KITUO CHA KUHIFADHI TAARIFA ZA MAFUTA NA GESI ASILIA** |
|---|---|
| MUDA | 2022-2027 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 43,360,000,000** |
| LENGO KUU | Kujenga kituo cha kudumu cha uhifadhi na usimamizi wa taarifa za mafuta na gesi asilia |
| FEDHA ZILIZOTEGWA KWA AJILI YA MRADI MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | Jumla ya **TZS 5,000,000,000** zimetengwa kutoka kutoka katika fedha za maendeleo za SMZ |
| Malengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023:<br>3) Ununuzi wa vifaa na uandaaji wa mifumo ya uhifadhi na usimamizi wa taarifa za mafuta na gesi asilia.<br>4) Kutoa mafunzo kwa wataalamu kuhusu usimamizi wa taarifa wa mafuta na gesi asilia.<br>5) Kufanya matengenezo ya jengo kwa ajili ya uhifadhi wa taarifa.<br>6) Kusafirisha taarifa za mafuta na gesi asilia kutoka PURA kuja ZPRA. | |

**KIAMBATISHO NAM 8L: MRADI WA UJENZI WA BOHARI YA GESI (NATURAL GAS/LPG STORAGE FACILITY) PAMOJA NA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI WA GESI**

| **JINA LAMRADI** | **MRADI WA UJENZI WA BOHARI YA GESI PAMOJA NA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI WA GESI** |
|---|---|
| MUDA | 2022-2026 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 70,000,000,000** |
| LENGO KUU | Uingizaji na usambazaji wa gesi kwa uuzaji wa watumiaji wa majumbani, mahoteli na maeneo mengine ya uzalishaji. |
| FEDHA ZILIZOTEGWA KWA AJILI YA MRADI MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | Jumla ya **TZS 2,000,000,000** zimetengwa kutoka kutoka katika fedha za maendeleo za SMZ |
| Malengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023:<br>1) Utaarishaji wa upembuzi yakinifu (feasibilty study)<br>2) Usanifu na michoro ya ujenzi wa Mradi<br>3) Ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia Gesi pamoja na usambazaji wa Gesi kwa wateja kwa hatua ya mwanzo (first phase). | |

**KIAMBATISHO NAM 8M: MRADI WA UJENZI WA BOHARI YA MAFUTA (BULK STORAGE FACILITIES) PAMOJA NA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI WA MAFUTA**

| JINA LAMRADI | MRADI WA UJENZI WA BOHARI YA MAFUTA PAMOJA NA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI WA MAFUTA |
|---|---|
| MUDA | 2022-2026 |
| JUMLA YA GHARAMA | **TZS 60,000,000,000** |
| LENGO KUU | Uingizaji kwa pamoja wa Mafuta pamoja na usambazaji kwa makampuni ya ndani ya mafuta. |
| FEDHA ZILIZOTEGWA KWA AJILI YA MRADI MWAKA WA FEDHA 2022/2023 | Jumla ya **TZS 4,000,000,000** zimetengwa kutoka kutoka katika fedha za maendeleo za SMZ |
| Malengo kwa mwaka wa fedha 2022/2023:<br>1) Utaarishaji wa upembuzi yakinifu (feasibilty study)<br>2) Upimaji na utaarishaji wa eneo<br>3) Ujenzi wa matangi ya kuhifadhia mafuta (50,000MT) | |